Nipashe
Jumanne Desemba 24, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581900
www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII
Nipashe digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0677 020 710 LIKE & FOLLOW US
epaper.ippmedia.com MIAKA 30 Nipashe Mwanga wa Jamii www.ippmedia.com

# Ujumbe wa Bagonza kwa wanasiasa na matajiri



• **Hajawaacha** manabii, bodaboda, wakulima maskini... *Ukurasa 2*



Moja ya nyumba 25 zilizobomoka kutokana na mvua inayoendelea kunyesha wilayani Same, mkoani Kilimanjaro. Watu sita wameripotiwa kufariki dunia. **PICHA: IDDA MUSHI**

# Mvua yaua watu sita, yabomoa nyumba 25

UK. 2

UKURASA WA 3

**Bingwa** Muhimbili: Kunywa maji kupitiliza au kunywa kidogo kunadhuru





UKURASA WA 3

**Chalamila** asema biashara Kariakoo rasmi kuwa saa 24 kuanzia Januari

UKURASA WA 4

**Washangaa** utata wanaohukumiwa kesi ukatili kijinsia huonekana uraiani



## Gari la DC lapigwa mawe, nyumba za viongozi kijijini zavunjwa, 32 watiwa mbaroni

UKURASA 18

**MICHEZO** **RAMOVIC: WACHEZAJI YANGA WANANIELEWA** UK.24 **MAONI,** UK.6

KRISMASI, MWAKA MPYA

# Ujumbe wa Bagonza kwa wanasiasa, matajiri

**Na Mwandishi Wetu**

ASKOFU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Karagwe, Benson Bagonza katika salamu zake za Krismasi na Mwaka Mpya 2025, ametoa ujumbe maalumu kwa matajiri na wanasiasa.

Katika salama zake hizo, Askofu Bagonza anasifika kwa kutoa maandiko yaliyojaa fikra tunduizi, anatoa wito kwa jamii, hasa matajiri "kuwageukia waliowasababishia utajiri wao ili nao wanufaike".

Kwa viongozi wa kisiasa, Askofu Bagonza ana ujumbe maalumu kwa aliowaita "viongozi wa kisiasa ambao hupatikana kwa kupigiwa kura", akisema "wapigakura maskini ndio huwatengeneza viongozi matajiri, ingawa wao husalia na umaskini".

Askofu Bagonza anasema katika andishi lake hilo: "...Bwana wetu Yesu Kristo, jinsi alivyokuwa maskini kwa ajili yenu; ingawa alikuwa tajiri, ili kwamba ninyi mpate kuwa matajiri kwa umaskini wake (ananukuu kitabu cha 2Kor 8:9 katika Biblia).

"Habari za maskini kutajirisha matajiri si ngeni kwetu. Tumewaona wakulima maskini wakitajirisha matajiri, waumini maskini wakiwatajirisha wahubiri. Bodaboda maskini wakiwatajirisha wauza pikipiki na maaskari barabarani.

"Wapigakura maskini wakitengeneza viongozi matajiri. Lakini maskini hawa hatuwezi kuwaita kuwa ni Yesu Kristo."

Askofu Bagonza anasema matajiri hawaonekani kuwatajirisha maskini. Badala yake kinachoonekana ni matajiri wanaodhani wana bidii na akili na maskini kuambiwa ni wavivu na hawana akili.

"Kwao hawa matajiri, kutajirika ni akili na ujanja. Hawa matajiri huwaona maskini kuwa ni wavivu na wasio na akili. Ukweli ni kwamba, utajiri na umaskini vina uhusiano wa karibu sana na mara nyingi uhusiano huu umejengwa katika unyonyaji.

"Kuzaliwa kwa Yesu kulileta picha tofauti. Yeye alikuwa tajiri, ili maskini wawe matajiri na alizaliwa katika hali ya umaskini, ili sisi tuwe matajiri. Maskini na matajiri wote wana nafasi katika kuzaliwa kwa Yesu.

"Lakini kwa namna ya pekee, Yesu alizaliwa kwa ajili ya waliokosa tumaini na kukosa mtetezi. Jamii yetu inalo la kujifunza kutoka Yesu Kristo. Tunaalikwa kumtazama Yesu katika sura ya watu wanateseka." Askofu Bagonza anataka watu wamtazame Yesu katika sura ya Mpalestina anayeteketezwa na mabomu ya nchi tajiri. Wamtazame Yesu kama mtu wa Ukraine anayekaangwa kwa mabomu ya Russia.

"Mtazame Yesu kama mwanaharakati anayepigania haki za kidemokrasia, anayetekwa na kupotezwa kama gaidi. Mtazame Yesu kama mtu maskini anayelazimika kununua haki zake katika ofisi za umma.

"Mtazame Yesu kama mwananchi maskini anayelazimika kununua uponyaji na wokovu wake. Mtazame Yesu kama mtu asiye mwanachama wa chama chochote anayepoteza haki ya kuchaguliwa kuwa kiongozi na kuishia kuwachagua wengine wamwongoze.

"Na haya yanapotokea, mtazame Yesu katika sura ya jamii inayokosa haki wakati watu wote wako kimya. Kwa umaskini wake na utajiri wake, Yesu Kristo amezaliwa kwetu. Yeye ni mtawala wa haki.

"Kwake hakuna mizengwe wala hila. Anatualika sote tumpokee na kumpeleka nyumbani kwetu, ofisini kwetu na kila mahali. Ninawatakia Noel njema na Mwaka Mpya wa 2025," Askofu Bagonza anahitimisha andishi lake la salamu za Krismasi na Mwaka Mpya.

**ASKOFU MWAMAKULA**

Naye Askofu Mkuu wa Kanisa la Moravian la Uamsho Tanzania na Afrika Mashariki, Emmaus Mwamakula katika ujumbe wake wa Krismasi na Mwaka Mpya, amegusia masuala ya utekaji, ukosefu wa ajira na kupanda kwa gharama za maisha.

"Tunaingia katika kusherehekea Sikukuu ya Krismasi wakati watu wetu wengi wapo katika hali ya shaka, hofu, hata kukata tamaa kwa mambo mengi sana," anasema.

Askofu huyo anasema hali ya usalama wa maisha ya watu na mali zao imezorota kwa kiasi kikubwa, vitendo vya utekaji na mauaji vimeweka jamii ya watanzania katika taharuki.

"Vijana wetu kadhaa waliotekwa katika kipindi cha miezi sita iliyopita hawajulikani waliko. Pia, hali ya usalama wa majengo nchini inaogopesha, moto unaunguza majengo huku mengine yakiporomoka na uwezo wa uokozi ni mdogo sana," anasema.

Askofu Mwamakula anasema ukosefu wa ajira nchini umekuwa janga linalotishia ustawi wa vijana.

Anasema uhalifu wa kisiasa unaonekana kuhalalishwa na watu wenye mamlaka kiasi cha kusababisha hata kufanyika mambo yasiyo ya uhalali katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka huu.


**NOTIFICATION TO THE DEPOSITORS, CREDITOR, BORROWERS & CUSTOMERS OF TRANSFER OF THEIR ACCOUNTS FROM CANARA BANK (TANZANIA) LIMITED TO EXIM BANK TANZANIA LIMITED**

Reference is hereby made to the Notice of Transfer of Assets and Liabilities dated September 26, 2024 which was published in the Daily News and Mwananchi newspapers on September 26, 2024, pursuant to Section 4 of the Transfer of Businesses (Protection of Creditors) Act in regard to the then proposed transfer by CANARA BANK(Tanzania) Limited (CBTL) of its assets and liabilities to Exim Bank Tanzania Limited (Exim Bank), subject to the obtaining of regulatory approvals.

**NOTICE** is hereby given to you, as Creditor/Depositor/ BORROWER & CUSTOMER, jointly by CBTL and Exim Bank that post getting all the regulatory approvals, the transfer has taken place on December 20, 2024 after business hours.

Signed on behalf of CBTL (Transferor) by:

Names: Rajshekhar Somashetty

Designation: MD & CEO

Signature:

Date: 23/12/2024

CANARA BANK (T) LIMITED TANZANIA DAR-ES-SALAAM

Signed on behalf of Exim Bank (Transferee) by:

Names: SUMIT SHEKHAR

Designation: HEAD - STRATEGIC MATTERS & SUBSIDIARIES.

Signature:

Date: 23/12/2024



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI**

**TANGAZO LA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MIKOA YA IRINGA, MBEYA NA DODOMA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA.**

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza unafanyika katika Mikoa ya Iringa, Mbeya na Dodoma katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapwa tarehe 27 Desemba, 2024 hadi 02 Januari, 2025. Zoezi la uboreshaji wa Daftari linafanyika kwa siku saba kwa kila kituo katika Mikoa hiyo.

1. **SIKU:** Uboreshaji unaanza siku ya Ijumaa tarehe 27 Desemba, 2024 hadi Alhamisi tarehe 02 Januari, 2025.
2. **VITUO:** Uboreshaji unafanyika katika vituo vilivyopo kwenye Mitaa, vijiji na vitongoji.
3. **MUDA:** Vituo vinafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni.

**Uboreshaji unahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa Miaka 18 na zaidi na hawakuwahi kuandikishwa hapo awali.
2. Kuandikisha Wapiga kura ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.
3. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi
4. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
5. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
6. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume www.inec.go.tz au anuani ya ovrs.inec.go.tz kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la kata kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo watakwenda nayo kituo cha kujiandikisha ili kukamilisha taratibu na kupata kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni.
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo.
- Mpiga Kura ambaye ana simu ndogo maarufu kama kitochi au kiswaswadu anaweza kuingia kwenye mfumo huo kwa kupiga *152*00#. Kisha, atachagua Namba 8 na kubonyeza, baada ya hapo atachagua namba 2 na kubonyeza, Kisha atachagua Namba 3 (Tume Huru ya Uchaguzi) na hapo, atapata huduma namba moja hadi nne. Atachagua huduma anayoitaka kati ya hizo nne. Hatimaye, atapata namba ya utambulisho (token number) atakayokwenda nayo kituoni kukamilisha mchakato wa kupata kadi ya mpiga kura.
- Mpiga kura anaweza pia kuwasiliana moja kwa moja na Maafisa wa Tume waliopo katika Kituo cha Huduma kwa Mpiga Kura kwa kupiga namba 0800112100 bila malipo.
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali, hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

**KUJIANDIKISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA**

**Limetolewa tarehe 19 Desemba, 2024 na:**

**Saida Hilal Mohammed**
**KAIMU MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

218302902


## Mvua yaua watu sita, nyumba 25 zabomolewa

**Na Idda Mushi,** SAME

WATU sita wamefariki dunia huku nyumba 25 zikibomoka sambamba na uharibifu wa mazao na miundombinu ya barabara wilayani Same, mkoani Kilimanjaro kutokana na mvua inayoendelea kunyesha.

Mwenyekiti wa Kamati ya Usalama ya Wilaya ya Same, Mkuu wa Wilaya hiyo, Kasilda Mgeni, aliwaambia waandishi wa habari wilayani humo jana kuwa hadi kufikia asubuhi ya jana, mvua hiyo imeleta madhara hayo.

Alisema miundombinu ikiwamo ya barabara hasa zinazoelekea kata za milimani imeharibiwa na kufanya baadhi ya maeneo kutofikika kwa urahisi.

Alitumia fursa hiyo kutoa pole kwa ndugu na jamaa walioathiriwa na majanga hayo yaliyosababishwa na mvua kubwa inayoendelea kunyesha wilayani humo.

Kwa mujibu wa taarifa ya kamati ya maafa ya wilaya hiyo, maeneo yaliyoathiriwa zaidi ni pamoja na kata za Msindo, Vuje, Bombo, Mtii na Maore ambako serikali inaendelea kufanya tathmini kupitia kamati ya maafa wilaya ili kujua ukubwa wa athari za mafuriko hayo na taarifa zake zipelekwe ofisi ya mkoa kwa ajili ya kufikishwa kwenye Ofisi ya Waziri Mkuu kwa hatua zaidi.

Mkuu wa Wilaya huyo aliwataka wananchi kuendelea kuwa na tahadhari ikiwamo kuhama kwa muda katika maeneo hatarishi ili kuepusha madhara zaidi ya kibinadamu na mazingira.

Mgeni akawaasa wananchi walio katika maeneo yaliyokumbwa na maafa kuwa watulivu wakati huu ambao serikali inaendelea na tathmini ya athari ya mafuriko.

"Mipango mbalimbali inaendelea kufanywa ili kuhakikisha miundombinu yote iliyoharibiwa na mvua inarejeshwa katika hali yake," alisema Mkuu wa Wilaya.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji mkoani Kilimanjaro, Mkaguzi Msaidizi Jeremiah Mkomagi aliwataja waliofariki dunia ni Joyce Elifuraha (57) na mumewe Elifuraha Elienea (59), wakazi wa kijiji cha Mjema.

Wengine ni Hamu Ally (76), mkazi wa kijiji cha Miombo, Kata ya Mtii; Elibariki Fanuel (48), mkazi wa kijiji cha Vuje, Lazaro Saikon (35), mkazi wa kijiji cha Mheza na Eliakunda Elisafi (69), mkazi wa kijiji cha Duma.

## Biashara Soko la Kariakoo sasa saa 24

Na Elizabeth Zaya

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, amesema kuanzia Januari mwakani shughuli za ufanyaji biashara katika Soko la Kimataifa la Kariakoo jijini Dar es Salaam zitakuwa wazi kwa saa 24.

Alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu masuala mbalimbali.

Chalamila alisema uzinduzi rasmi kwa ajili ya kuanza utaratibu huo wa biashara katika soko hilo utafanyika mwanzoni mwa mwaka 2025.

Alisema tayari serikali imeanza kuboresha miundombinu ya soko hilo ikiwa ni pamoja na kuweka kamera za usalama, taa za barabarani na vifaa vingine muhimu ili kuhakikisha mpango huo unafanikiwa.

"Dar es Salaam ina uwezo wa kuendesha biashara saa 24, Kariakoo kama soko linalohudumia mataifa jirani, litachangia kuimarisha uchumi wa mkoa na kuongeza nafasi za ajira," alisema Chalamila.

"Na tunataka mpango huu utumike kuimarisha amani na kuboresha Jiji la Dar es Salaam kama kitovu cha biashara kwa nchi jirani kama Rwanda, Burundi, Comoro na Uganda."

Kadhalika, alisema katika kipindi hiki cha msimu wa sikukuu, alisisitiza umuhimu wa wananchi kushirikiana na vyombo vya usalama ili kudumisha amani.

Alisema Jeshi la Polisi limejipanga kuhakikisha usalama wa wananchi unaimarishwa katika kipindi chote cha sikukuu na kutoa wito kwa wananchi kutembea na vitambulisho ili kurahisisha utambuzi wao katika matukio ya dharura.

Kadhalika, aliwataka wananchi kuepuka kusambaza uvumi usio na msingi kwa sababu kufanya hivyo wanasababisha taharuki kwenye jamii.

"Niwaonye wananchi katika mkoa huu wa Dar es Salaam, waepuke kusambaza taarifa za uvumi zisizo na msingi, taarifa zisizo sahihi zinaweza kusababisha hofu isiyo na lazima na kuathiri usalama kwa jamii," alisema Chalamila.

Pia, aliwapongeza waandishi wa habari kwa mchango wao katika kufikisha taarifa kwa jamii na kusaidia kujenga taifa kupitia ukosoaji wenye lengo la kujenga na kuwahimiza kuwa waangalifu na taarifa wanazozitoa, hususani zinazohusu matukio ya utekaji akisisitiza umuhimu wa kuthibitisha usahihi wa taarifa kabla ya kuzisambaza.

Vilevile, alitoa angalizo za usahihi na kuthibitisha taarifa zinazotolewa akirejea taarifa za matukio ya utekaji zilizoripotiwa hivi karibuni.

# Bingwa Muhimbili: Ukinywa maji kidogo au kuzidisha unadhurika

Na Christina Mwakangale

BINGWA wa Magonjwa ya Figo na Mfumo wa Mkojo katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH), Dk. Jonathan Mngumi, amesema unywaji duni wa maji au uliopitiliza mahitaji mwilini, huathiri mfumo wa mkojo, figo na kibofu.

Amesema unywaji maji kwa siku hutakiwa kuwa wa wastani kulingana na kazi anayofanya mtu, lakini ni lazima kwanza mtu asikilize kiu yake na si vinginevyo.

Bingwa huyo ambaye ni Mkuu wa Kitengo cha Figo MNH, ameyasema hayo katika mazungumzo na Nipashe kuhusu unywaji maji, akisema kiasi cha maji kwa mtu anayefanya kazi nzito hasa juani, anayetoka jasho jingi, ni kati ya lita tatu hadi tano kwa siku.

"Kwa wastani mtu mzima anayefanya kazi nzito juani au kazi ya kutoka jasho jingi anashauriwa kunywa maji kati ya lita tatu hadi tano kwa siku kulingana na kiwango cha jasho na unyevunyevu wa mazingira.

"Ishara za mwili, ikiwa mtu anajisikia kiu sana au mkojo wake ni wa rangi ya njano iliyokolea, ni dalili ya ukosefu wa maji mwilini na anapaswa kuongeza unywaji maji," anasema.

Mtaalamu huyo anasema unywaji maji usio sahihi kwenye viungo vya mwili, pia unywaji duni, huchangia kuathiri viungo kadhaa muhimu kama vile figo, ngozi, moyo na ubongo.

"Wastani wa kujisaidia haja ndogo kwa saa 12 mpaka 24 kwa mtu mwenye afya njema ni mara nne hadi saba kwa siku, ni kawaida sawa na kila baada ya saa tatu hadi nne.

"Kujisaidia haja ndogo kwa saa 12 ni mara mbili hadi nne ndani ya muda huo. Kwa saa 24 kujisaidia ni mara nne hadi saba, kulingana na kiwango cha unywaji maji na shughuli za mwili," anafafanua.

Bingwa huyo pia anaonya unywaji maji kwa kiwango kilichopitiliza, akiwa na maelezo kuwa kuna madhara iwapo mtu atakunywa maji mengi kwa muda mfupi kiasi kwamba mwili hauwezi kuyatoa au kuyasawazisha kwa njia ya mkojo.

"Kwa watu wengi wazima, kunywa zaidi ya lita tano za maji kwa siku au zaidi ya lita moja au lita moja nusu kwa saa kunaweza kuwa hatari," anaonya.

***USIKOSE MAKALA KUHUSU SUALA HILI KATIKA GAZETI HILI KESHOKUTWA, ALHAMISI**

*Kwamaoni:+255677020701*
*Email:customerrelations@guardian*



Katibu Tawala Mkoa wa Kigoma, Hassan Rugwa (kushoto), akipokea jiko la gesi kutoka kwa mwakilishi wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Viwanda (UNIDO), Doroth Kitutu, jana wakati shirika hilo lilipotoa majiko ya gesi yenye thamani ya Sh. milioni 14 kwa Shule ya Sekondari ya Wasichana Uvinza kwa lengo la kuunga mkono vita dhidi ya matumizi ya nishati chafu nchini. **PICHA : ADELA MADYANE**

# Ajali yakatisha uhai wa Mkurugenzi Hazina

Na Joyce Lameck

MATUKIO ya ajali mwishoni mwa mwaka yameendelea kuacha vilio na majonzi katika jamii baada ya juzi aliyekuwa Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu Ofisi ya Msajili wa Hazina, Amos Nnko, kufariki dunia kwa ajali ya gari.

Nnko amefariki dunia katika ajali ya gari iliyotokea Desemba 22 huko Same, mkoani Kilimanjaro. Katika ajali hiyo, binti yake wa kwanza, Maureen Nnko naye alifariki dunia.

Taarifa iliyotolewa jana na Msajili wa Hazina, Nehemiah Mchechu ilieleza" "Msajili wa Hazina anasikitika kutangaza kifo cha Amos Nnko aliyekuwa Mkurugenzi wa Utawala na Usimamizi wa Rasilimaliwatu kilichosababishwa na ajali ya gari iliyotokea maeneo ya Same, mkoani Kilimanjaro."

Taarifa hiyo pia ilieleza kuwa mke wa marehemu, Agnes Nnko na watoto wao Marilyn, Melvin na mwanafamilia mwingine aitwaye Sylvana, wanapatiwa matibabu katika Hospitali ya Kanda ya Kaskazini (KCMC) na Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Kilimanjaro (Mawenzi).

Ilielezwa katika taarifa hiyo kuwa mipango ya mazishi inaendelea kuratibiwa na familia ya marehemu kwa kushirikiana na Ofisi ya Msajili wa Hazina.

Hivi karibuni kumekuwa na mfululizo wa matukio ya ajali za barabarani ambazo zimesababisha vifo vya watanzania wengi.

Desemba 18, mwaka huu, huko Mikese, mkoani Morogoro, gari aina ya Coaster iligongana na lori la mizigo na kusababisha vifo vya watu 15 na kujeruhi saba. Baadaye mmoja wa majeruhi hao alifariki dunia wakati anapatiwa matibabu katika Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) na kufanya idadi ya vifo kuwa vya watu 16.

Juzi katika kijiji cha Kabukome, Kata ya Nyarubungo, wilayani Biharamulo, basi la kampuni ya Capro One lenye namba za usajili T857 DHW lilifeli breki katika mteremko na kurudi nyuma kisha kupinduka na kusababisha vifo vya watu 11 na wengine 16 kujeruhiwa.

Kutokana na matukio hayo, Rais Samia Suluhu Hassan aliagiza Jeshi la Polisi kuwa na mfumo wa leseni za udereva utakaowapunguzia alama madereva wanaofanya makosa yenye kuhatarisha usalama na uhai barabarani.



Skani hapa kutembelea chaneli yetu

# Washangaa watuhumiwa ukatili kuwa uraiani

Na Maulid Mmbaga

WANAHARAKATI wanaopinga unyanyasaji wa kijinsia, ukatili na rushwa ya ngono nchini wamesema licha ya kutumia muda na nguvu kubwa katika kukemea vitendo hivyo na hata kuwapeleka mahakamani watuhumiwa, wamekuwa wakishangazwa kuwaona wahusika wakitamba mitaani baada ya kesi kuisha.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Wanawake katika Jitihada za Kimaendeleo (WAJIKI), Janeth Mawinza, alisema juzi kuwa moja ya mambo yanayowakatisha tamaa na kuwarudisha nyuma ni kuona kesi za vitendo vya ukatili zikishindwa kumalizika katika hatua nzuri.

Alisema wamekuwa wakifuatilia kesi mbalimbali kwa kushirikiana na wadau kwa kufuata taratibu zote za kisheria, lakini kesi hizo zimekuwa hazifiki mwisho unaoridhisha, jambo ambalo linaweza kuhatarisha jamii na kutowatendea haki waathirika.

"Tunafuatilia kesi mbalimbali japo umalizikaji umekuwa changamoto, kuna ambazo zinaisha lakini inaumiza pale ambapo uamuzi umefanyika, mtoto aliyetendwa vitendo vya ukatili ameshinda, lakini mhusika yuko nje, hilo kwetu tunaona ni tatizo kubwa.

"Sisi tunafuatilia tunampeleka mtuhumiwa mahakamani na ameonekana kuwa ana hatia, anatakiwa kwenda jela, aidha miaka 30 au kifungo cha maisha, lakini tunajiuliza kwanini anabaki nje? Tunatengeneza nini? Tunajiaminisha vipi kwamba hatawadhuru wengine?

"Tunategemea kwamba wanaokutwa na hatia wanapopelekwa gerezani wanakwenda kupata mafunzo ya kumfanya akirudi uraiani asifanye tena hivyo vitendo, sasa kama anabaki uraiani inaleta picha gani? Hadi sasa tumeona kesi mbili ambazo mtuhumiwa anahukumiwa lakini anabaki nje," alisema Janeth.

Alisema kuwa kila wanapojaribu kufuatilia, wahusika hao wamekuwa wakihama maeneo mbalimbali ili kujificha licha ya kwamba hukumu zao zilishatolewa. Kutokana na ushirikiano wanaopata kutoka kwa jamii, inawasaidia kupata taarifa za mienendo ya wahusika hao wa vitendo vya ukatili.

"Jamii sasa imeshafunguka, wanajamii wanavunja ukimya lakini huku kwenye umalizikaji mnyororo hauunganiki vizuri, unakatikakatika, shida iko wapi? Kutokana na hali hii tulienda kutoa taarifa Ustawi Halmashauri ya Kinondoni tukakabidhiwa kwa afande lakini kuzungushwa kulikuwa kwingi.

"Pamoja na kufanya kazi kwetu kuamsha jamii iseme, lakini kuna mahali wanarudishwa nyuma, leo nikiona huyu kaenda hakuna kilichofanyika, tunawafanya watu wanyamaze lakini tunaendelea kupaza sauti kupitia vyombo vya habari ili mamlaka isikie," alisema Janeth.

Mjumbe wa WAJIKI, Hancy Obote, alisema wale ambao ni wakosaji wanawaona wao kama maadui wakubwa, hata kuwanyooshea vidole na wakati mwingine wanawatishia, mazingira ambayo yalisababisha kipindi fulani mkurugenzi wao apelekwe kukaa mahali salama.

Alisema hali hiyo inawapa shida na kusababisha wakati mwingine kufikiria kukata tamaa.

"Jambo lingine ni kwa wenzetu wenye mamlaka ambao sisi tunasema tunafanya uchechemuzi lakini watendaji ni wao, japo wakati mwingine wanaleta kujuana, rushwa na ubabe.

"Mwisho wa siku anayetumia nguvu nyingi na kuumia ni wewe, lakini wao maisha yanaendelea, kwa sababu tunapambana kesi zinakwenda mahakamani lakini zinaisha mtuhumiwa anaonekana mtaani, hata jamii inakosa imani, wanaona ni yaleyale, hapa tunatengeneza bomu, mazingira haya yanaweza kusababisha uvunjifu wa amani," alisema Obote.

Mkurugenzi wa WAJIKI, Janeth, alitoa tahadhari kuwa vyombo vya uamuzi visiposimama na kuwasaidia walalamikaji, vitakuwa wanafanya kitu cha hatari kwa kuwa watanyamazisha sauti za jamii.



Mkurugenzi wa Jumba la Makumbusho la Iringa (IRINGA BOMA) ambaye ni Meneja wa Mradi wa Fahari Yetu, Jimson Sanga (kulia), akiwaelekeza jambo wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) idara ya utalii walipotembelea Makumbusho hiyo juzi kujifunza. **PICHA: FRANCIS GODWIN.**

## Chongolo awapasha viongozi Dira ya Maendeleo ya Taifa

**Na Mwandishi Wetu,** NJOMBE

VIONGOZI wa kisiasa na serikali mkoani hapa wametakiwa kutafsiri Dira ya Maendeleo ya Taifa ya Mwaka 2025 hadi 2050 kwa manufaa ya wananchi.

Wito huo ulitolewa juzi na Mjumbe wa Mkutano Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM)Taifa ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Songwe, Daniel Chongolo wakati wa hafla ya uzinduzi yo hamasa ya uandikishwaji katika daftari la mpigakura Wilaya ya Njombe.

Chongolo alisema moja ya kosa ambalo limewahi kufanyika ni kutoitafsiri dira hiyo kutokana na changamoto za Mkoa wa Njombe.

Alisema viongozi hao wanatakiwa kujipanga kutafsiri dira hiyo kwa kuihusisha na namna ambavyo mkoa huo unaweza kunufaika na fursa za kiuchumi kutokana na kuwa lango la kimataifa biashara kwa kuwa nchi nyingi zipitisha mizigo hasa Makambako.

"Sasa hivi tuna dira mpya ambayo inaanza mwaka kesho, itaenda kwa miaka 25 tujipange kuitafsiri kwa sura hiyo, Njombe hili ni lango la mikoa mingi na ni lango la mataifa, hakuna mzigo unaotoka Zambia bila ya kupita hapa," alisema Chongolo.

Aliwataka viongozi hao kuachana na tabia ya ubinafsi kwa kuwawezesha vijana kupata fursa za kiuchumi ili kukuza kipato chao.

Awali Mwenyekiti wa Umoja wa Vijana wa Chama hicho Wilaya ya Njombe, Erick Ngole, aliwataka vijana kuhamasisha wananchi kushiriki katika uboreshaji wa daftari la kudumu la mpigakura ili kushiriki Uchaguzi Mkuu wa 2025.

# JKCI kuwapima, kuwatibu watu 20,000 bila malipo

Na Christina Mwakangale

ZAIDI ya wananchi 20,000 wanatarajiwa kupatiwa huduma za upimaji na matibabu ya magonjwa yasiyoambukizwa, yakiwamo magonjwa ya moyo, presha na kisukari, katika maeneo mbalimbali nchini kufikia mwaka 2025.

Huduma hiyo inatekelezwa na Taasisi ya Moyo ya Jakaya Kikwete (JKCI) kwa ufadhili wa Rais Samia Suluhu Hassan kupitia mpango wa 'Dk. Samia Suluhu Tiba Mkoba' unaowawezesha madaktari bingwa wa taasisi hiyo kutoa huduma bila malipo katika mikoa mbalimbali nchini.

Mkurugenzi Mtendaji wa JKCI, Dk. Peter Kisenge, alisema kuwa hadi sasa, wananchi 18,000 kutoka mikoa 17 wamepatiwa huduma hiyo ikiwa ni pamoja na upimaji na matibabu kwa wale waliobainika na magonjwa hayo.

Dk. Kisenge alifafanua kwamba huduma hiyo ilianzishwa baada ya Rais Samia kuagiza wananchi wapatiwe vipimo na matibabu katika maeneo yao, ili kupunguza gharama na muda unaopotea katika hospitali kubwa.

"Kwa kuanzisha huduma ya Dk. Samia Suluhu Tiba Mkoba Januari mwaka jana, tumeweza kuwafikia wananchi wengi na kusaidia kuimarisha afya zao, mwitikio wa wananchi umekuwa mkubwa," alisema Dk. Kisenge.

Aliongeza kuwa huduma hiyo imetekelezwa kwa kuwafikia makundi mbalimbali, ikiwa ni pamoja na waandishi wa habari ambao wamepata fursa ya kupima afya zao bure na kusaidia kutoa elimu kuhusu umuhimu wa kupima afya.

Alisema wasanii kutoka sekta ya uigizaji, uimbaji na uchekeshaji pia wamejitokeza kupima afya zao ili kujua hali zao na kupata matibabu mapema.

Mkurugenzi wa JKCI-Dar Group na Bingwa Mbobezi wa Magonjwa ya Moyo, Dk. Tulizo Shemu, alisema wataendelea kuwahamasisha wasanii wote nchini kupima afya zao mapema ili kusaidia kugundua viashiria vya magonjwa yasiyoambukiza na kupata tiba mapema.

"Ni muhimu kwa wasanii kujitokeza kupima afya zao mapema, kwani inasaidia kujua hali zao za kiafya, hususan viashiria vya magonjwa yasiyoambukizwa na hivyo kupata matibabu kwa wakati," alisema Dk. Shemu.

Kaimu Katibu Mtendaji wa Bodi ya Filamu Tanzania (TFB), Dk. Gelvas Kasiga alisema utaratibu huo utasaidia wasanii kujua afya zao na kufanya kazi kwa uhuru huku wakifanikisha malengo waliyojiwekea.

Daktari wa Kituo cha JKCI Kawe, Dk. Johnstone Ndabila, alisema wanaendelea kuwahamasisha wananchi kujitokeza kwa wingi kupima afya zao katika vituo mbalimbali vya kutoa huduma za matibabu ya magonjwa yasiyoambukizwa, yakiwamo maradhi ya moyo, kisukari na presha.

TANGAZO

LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

# EXPRESSION OF INTEREST FOR THE PROVISION AND SUPPLY OF GOODS AND SERVICES (2025–2027)

The Legal and Human Rights Centre (LHRC), a non-profit, non-governmental, and non-partisan human rights organization, was established in 1995 to promote a just and equitable society. LHRC operates through funding from various development partners and is currently implementing its 2025–2027 Operational Plan.

LHRC invites eligible, reliable, and well-established service providers to submit Expressions of Interest (EOI) for the provision of goods and services in the categories listed below:

| S/N | Category | Description |
|---|---|---|
| LHRC/2024/1 | **Conference and Accommodation Services** | Hotels and conference facilities |
| LHRC/2024/2 | **Building Maintenance and Materials Supply** | Masonry, painting, plumbing, electrical works, signage, roofing, landscaping, etc. |
| LHRC/2024/3 | **Catering Services** | Catering for events and meetings |
| LHRC/2024/4 | **Courier and Mail Delivery Services** | Mail and parcel delivery |
| LHRC/2024/5 | **Cleaning and Pest Control Services** | Cleaning, fumigation, and pest control |
| LHRC/2024/6 | **Insurance Services** | Health and life insurance, building, travel, and equipment insurance (e.g., laptops) |
| LHRC/2024/7 | **Audit and Assurance Services** | Internal and external audit |
| LHRC/2024/8 | **Professional and Consultancy Services** | Tax advisory, resource mobilization, training, facilitation, media monitoring, litigation, and program development |
| LHRC/2024/9 | **Office Furniture and Fittings Supply and Maintenance** | Office furniture and fittings |
| LHRC/2024/10 | **Publication Services** | Editorial, typesetting, and printing |
| LHRC/2024/11 | **IT Infrastructure Supply, Installation, and Maintenance** | LAN, alarms, CCTV, and access control systems |
| LHRC/2024/12 | **Internet Services** | Internet and data connectivity |
| LHRC/2024/13 | **Creative and Marketing Services** | Branding, graphic design, social media management, and public relations |
| LHRC/2024/14 | **Office Stationery Supply** | Toners, papers, inks, pens, files, etc. |
| LHRC/2024/15 | **Air Conditioners, Refrigerators, and Generators Supply, Installation, and Maintenance** | Air conditioners, refrigerators, and generators |
| LHRC/2024/16 | **Translation and Interpretation Services** | Translation, interpretation, and sign language services |
| LHRC/2024/17 | **Logistics and Travel Services** | Air, road, rail, and water travel services |
| LHRC/2024/18 | **Fuel and Lubricants Supply** | Fuel and lubricants for vehicles and generators |
| LHRC/2024/19 | **Vehicle Maintenance Services** | Vehicle spare parts, repairs, and maintenance |
| LHRC/2024/20 | **Security Services** | Office and premises security |
| LHRC/2024/21 | **Fleet Management Services** | Vehicle tracking services |
| LHRC/2024/22 | **ICT Equipment and Software Supply and Maintenance** | Software, servers, computers, printers, scanners, mobile phones, etc. |
| LHRC/2024/23 | **Disaster Recovery Services** | Colocation and disaster recovery site infrastructure |
| LHRC/2024/24 | **File Scanning and Digital Archiving Services** | File scanning, indexing, and archiving |
| LHRC/2024/25 | **Audio-Visual Production Services** | Video and audio production, and graphic design |
| LHRC/2024/26 | **Event Management Services** | Ushering, protocol, moderation, and floor management |
| LHRC/2024/27 | **Event Decor and Rental Services** | Rental of chairs, tables, mobile toilets, flowers, balloons, and carpets |
| LHRC/2024/28 | **Human Resource and Recruitment Services** | Recruitment, training, and staff engagement |
| LHRC/2024/29 | **Building Construction Services** | Architectural designs, quantity surveying, and construction |
| LHRC/2024/30 | **Real Estate Management Services** | Real estate development and management |
| LHRC/2024/31 | **Public Auction Services** | Property and vehicle auctions |

**MODE OF SUBMISSION**

Interested suppliers may apply for one or more categories listed above. Separate applications must be submitted for each category, clearly indicating the category number.

Applications should be enclosed in a sealed envelope, clearly marked with the category number and type of service, and addressed to:

The Chairperson
LHRC Procurement Committee
P.O. BOX 75254
Dar es Salaam

Applications must be submitted to the LHRC Head Office by 6th January 2025.

---

**SHORTLISTING CRITERIA**

1. Articles of Association and valid business license.
2. Proof of payment of statutory obligations (e.g., Tax Clearance Certificate).
3. Minimum of three (3) years of relevant experience with references and recommendation letters from at least two clients.
4. Demonstrated capacity and ability to deliver the services.

Shortlisted service providers will receive tender documents to bid for the supply of goods and services as needed.

**NOTE:** The Legal and Human Rights Centre does not bind itself to pre qualify any supplier (s) or give reasons to its decision and is not obliged to accept the lowest or any tender.

183056

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Tunawatakia Krismasi njema yenye baraka

**KESHO** Wakristo wote duniani wanaadhimisha kumbukumbu ya kuzaliwa mwokozi wao Yesu Kristo.

Kumbukumbu hii ni muhimu kwa sababu duniani kote wanaadhimisha kwa kuanza kupamba mapema sehemu mbalimbali, iwe kwenye maduka makubwa, ofisi, sehemu za starehe barabarani ili kuashiria kuwa sikukuu hiyo imewadia.

Wanaojua umuhimu wa sikukuu hiyo huitumia kutoa zawadi kwa marafiki, ndugu na jamaa na makundi yasiyojiweza ili kuonesha ishara ya upendo.

Kwenye maduka mbalimbali bidhaa nyingi hupunguzwa bei ili kumwezesha kila mtu kumudu kununua mahitaji na kuweza kufurahia sikukuu hiyo kwa shangwe.

Kwa wafanyabiashara wanaofanya hivyo ni kuonesha kuwa wanawajali wateja wao na vilevile hupata baraka katika biashara zao na kuongeza mapato.

Hata hivyo, kwa baadhi ya wafanyabiashara hutumia kipindi hiki kujinufaisha zaidi badala ya kuwajali wateja wao.

Kipindi hiki hutumika kupandisha bidhaa bei hasa vyakula na mavazi na kuwaumiza wateja.

Wanafanya hivyo kwa kutambua kuwa lazima watu watanunua kwa sababu wapo katika uhitaji. Hiki ni kipindi ambacho wazazi wengi huingia kwenye mawazo kutokana na familia kutaka kununuliwa nguo mpya na vile vile kula chakula kizuri.

Wafanyabiashara hutumia mwanya huo kuhakikisha kuwa huo ndio muda wa mavuno kwao. Kwa mfano nguo iliyokuwa ikiuzwa Sh. 20,000 itapanda na kuwa Sh. 25,000 hadi 30,000.

Kwa upande wa chakula, kipimo cha sado moja ya nyanya ambayo ilikuwa inanunuliwa kwa Sh. 2,500 itapanda hadi Sh. 4,000.

Kilo moja ya nyama ambayo ilikuwa inanunuliwa kwa Sh. 8,000, sasa itapanda hadi Sh. 12,000.

Huu sio uungwana hata kidogo, kila mmoja anapenda siku kama hiyo kukaa na familia yake ale chakula nao chakula kizuri, lakini kwa ubinafsi wa kupenda fedha za haraka, mnawaumiza wenzenu.

Ni vigezo vipi vinavyosababisha bidhaa hizo kupanda ghafla wakati wa sikukuu na inapomalizika, bei zinarudi kama kawaida.

Ukiwauliza wafanyabiashara wanajibu kuwa eti gharama za usafirishaji kipindi cha sikukuu zinapanda. Zinapanda vipi wakati bei za dizeli na petroli ziko palepale, wakati bei hizo ndio huchukuliwa kama sababu ya kupanda kwa gharama.

Wafanyabiashara kueni na huruma na wenzenu, kumbukeni kuwa kipindi hiki ndicho cha kujitafutia thawabu kwa Mwenyezi Mungu.

Katika sikukuu hizi za mwisho wa mwaka kuna mambo mengi yanayojitokeza, hivyo ni lazima jamii iwe makini kulinda familia zao.

Watoto hupendelea kwenda fukwe za bahari kusherehekea, ni vizuri kuwa na uangalizi wa watu wazima ili kuepuka majanga.

Vile vile, kuna watu wanaosubiri familia zitoke kwenye nyumba zao halafu wao watumie muda huo kufanya uovu wa kuvunja nyumba hizo na kuiba mali. Jamii lazima iwe makini ihakikishe familia inapotoka inaacha mtu wa kuangalia.

Hiki sio kipindi cha kusherehekea kwa kufanya vurugu. Ni kipindi cha kufurahi kwa amani na kumshukuru Mungu kwa kuweza kukulinda mwaka mzima na kuiona tena siku hii.

Kuna wengine walitamani kufurahi katika siku hiyo, lakini sasa hivi ni wagonjwa wako vitandani wakipigania maisha.

Basi kwa waliobahatika kuwa salama ni kipindi cha kumshukuru Mungu kwa kutoa sadaka ili uendelee kubarikiwa.

**Tunawatakiwa wote maandalizi mema ya Krismasi na Mwaka Mpya 2025.**

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677 020 701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Sabato Kasika

# Wazazi na walezi andikisheni watoto

**SERIKALI** inatarajia kuandikisha watoto zaidi ya milioni 1.8 wa elimu ya awali na wengine milioni 1.7 watakaoanza darasa la kwanza mwaka ujao wa 2025. Kutokana na hilo, kinachoendelea ni kuhimiza wazazi na walezi kuwaandikisha watoto wao.

Wiki iliyopita, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa anawaagiza wazazi na walezi kutimiza wajibu wa kuwaandikisha watoto wao wote wenye umri wa kwenda shule badala ya kuwaacha wakauze maandazi, karanga na miwa mitaani.

Ninaamini uandikishaji wa sasa hauna lawama kama ilivyokuwa zamani ambapo baadhi ya wazazi na walezi walikuwa wakiwalaumu walimu wakuu kuwa wanatoza fedha za madawati wakati wa kuandikisha.

Baadhi ya wazazi na walezi huwa wanalalamika wakidai kuwa wanaombwa fedha, kwa ajili ya kununua madawati na kusababisha wasio nazo kushindwa kuwaandikisha watoto wao.

Akiwa katika ziara mkoani Simiyu Waziri Mkuu anawapa jukumu watendaji wa kata wote wakae na watendaji wa vijiji na mitaa kuwahimiza uandikishwaji wa watoto wenye umri wa kwenda shule, kwa kuwa kila mtoto wa Kitanzania anatakiwa kuwa shule.

Katika ufafanuzi wake anasema mtoto wa Kitanzania anatakiwa kwenda shule, kwa kuwa ameandaliwa utaratibu wa kupata elimu kuanzia chekechea, shule za msingi hadi sekondari.

Kwa maelekezo hayo ya serikali, ni vyema wazazi na walezi nao wakauzingatia kwa manufaa ya baadaye ya watoto wao badala ya kuwafanyisha kazi wakiwa hawajafikia umri wa kuingia katika ajira.

Ikumbukwe amewekeza kwenye upatikanaji wa elimu, kwa kutoa fedha za ujenzi wa shule, madarasa na mabweni, lakini pia inatoa elimu bure, ili kila mtoto wa Kitanzania apate fursa ya kusoma.

Kwa unafuu huo, ninadhani kila mzazi na mlezi ana wajibu wa kuhakikisha mtoto wake anapata elimu kwa kumnunulia mahitaji yote ya shule, kwani mzigo mwingine unabebwa na serikali.

Itakuwa ni jambo la kushangaza iwapo bado kutakuwa na baadhi ya watu ambao watashindwa kuwaandikisha watoto wao ili waanze elimu ya awali au msingi wakati elimu ikitolewa bure.

Hadi Waziri Mkuu kuwahimiza kuandikisha watoto, maana yake ni kwamba bado wapo wale ambao hawajaona umuhimu wa elimu. Watu wa aina hiyo wangesaidiwa kujua kuwa elimu ina manufaa makubwa.

Elimu ni zaidi ya kusoma, kuandika na kuhesabu, ni moja ya uwekezaji muhimu ambao nchi inaweza kufanya, husaidia watu kufanya kazi vizuri na inaweza kuunda fursa za ukuaji endelevu wa uchumi kwa siku zijazo.

Vilevile, elimu pia inawapa watu ujuzi muhimu na zana za kuwasaidia kujikimu wao wenyewe na watoto wao. Pia inasaidia kuwa na uwezo wa kujitegemea kifedha, lakini si hilo tu, pia inakufanya uwe na hekima zaidi ili uweze kufanya na kuchukua maamuzi binafsi.

Aidha, elimu huathiri zaidi uelewa wa watu wa tofauti kati ya mema na mabaya. Mtu aliyeelimika anafahamu vyema madhara ya matendo haramu lakini asiye na elimu ana uwezekano mdogo wa kushawishiwa kufanya jambo ambalo si sahihi au sahihi.

Maana yake ni kwamba, ikiwa umeelimishwa, unafahamu vyema haki zako, sheria na wajibu kwa ajili ya kuboresha jamii. Hivyo, elimu ni muhimu kwani pia huchangia katika maelewano ya kijamii na amani.

Lakini pia dunia inabadilika kila kukicha huku teknolojia mpya ikizidi kuibuliwa, hivyo bila elimu ni vigumu watoto kwenda na mabadiliko, lakini aliyeelimika itakuwa rahisi kwake kufahamu vizuri teknolojia.

Kwa mantiki hiyo wazazi na walezi wasibaki nyuma kwa kuwapa watoto vitu vidogo vidogo vya kuuza badala ya kuwaandikisha wakapate elimu ya kuwawezesha kupata elimu ya kuwasaidia katika maisha ya baadaye.

Pamoja na hayo, waandikishaji waepuke kurushiwa lawama ambazo hujitokeza kuwa huwatoza fedha wazazi na walezi wanapokwenda kuandikisha watoto wao na kufanya wengine washindwe kuwaandikisha.

Baadhi ya wazazi na walezi huwa wanalalamika wakidai kuwa wanaombwa fedha kwa ajili ya kununua madawati na kusababisha wasio nazo kushindwa kuwaandikisha watoto wao.

## Polisi yanasa madini bandia

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

JESHI la Polisi Mkoa wa Shinyanga limekamata madini bandia yadhaniwayo kuwa ya dhahabu zaidi ya gramu 250 na silaha aina ya gobore iliyokuwa imebebwa kwenye baiskeli.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Janeth Magomi, alitoa taarifa hiyo jana kwa vyombo vya habari baada ya msako waliofanya kuanzia Novemba 27 hadi Desemba 22, mwaka huu.

Alisema katika msako huo wamekuta watuhumiwa 81 na vielelezo mbalimbali, yakiwamo madini bandia gramu 250 yadhaniwayo kuwa ni dhahabu.

"Pia tumekamata silaha aina ya gobore katika kijiji cha Bugomba A, Ushetu wilayani Kahama ambako mtuhumiwa alikuwa ameibeba kwenye baiskeli na alipoona gari la polisi alikimbia na kuitelekeza. Tunaendelea kumsaka," alisema.

Kamanda Janeth alisema vielelezo vingine vilivyokamatwa ni pamoja na bangi gramu 9,000, mirungi mabunda tisa, pombe haramu aina ya gongo lita 113, sola panel saba, betri nne za sola, pikipiki 11, kadi tatu za pikipiki na antena nne za ving'amuzi.

Vingine ni redio mbili, baiskeli mbili, mashine moja ya bonanza, kamera moja na mitambo minne ya kutengeneza gongo.

Alisema kuwa kwa upande wa makosa ya usalama barabarani, wamekamata makosa 5,376, magari 3,767, bajaji na pikipiki 1,609 na wahusika waliwajibishwa na kulipa faini za papo kwa papo.

Katika hatua nyingine, Kamanda Janeth ametoa wito kwa wananchi kuendelea kutoa ushirikiano kwa kutoa taarifa za uhalifu, huku akiwakumbusha wazazi na walezi kuwa makini na watoto wao katika kipindi hiki cha sikukuu za mwisho wa mwaka.



Mwenyekiti wa Kamati Tendaji ya Ufuatiliaji wa Migogoro ya Ardhi Kitongoji cha Kingani, Kata ya Kisutu, Wilaya ya Bagamoyo mkoani Pwani, Dk. Mwajabu Loya, akionyesha nyaraka mbalimbali zinazohusiana na mgogoro wa ardhi katika eneo hilo, kwa waandishi wa habari na kuiomba serikali na vyombo vya dola kuingilia kati, ambapo anayedai kushinda kesi ya kuwa eneo hilo ni lake Ibrahim Sudi anawataka wakazi wa eneo hilo waondoke. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Majaliwa: Watoto wapelekwe shuleni, msiruhusu wauze maandazi, karanga

**Na Mwandishi Wetu,** MWANZA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amewataka wazazi wahakikishe wanawaandikisha watoto wote wenye umri wa kwenda shuleni badala ya kuwaacha wakauze maandazi, karanga na miwa.

Katika kutekeleza agizo lake hilo, Majaliwa amewataka watendaji wa kata kote nchini wakae na watendaji wa vijiji na mitaa ili kuwahimiza suala la uandikishaji watoto wenye umri wa kwenda shuleni.

"Mtoto wa kitanzania anatakiwa kwenda shuleni kwa sababu mtoto huyu leo ameandaliwa utaratibu wa kuanzia chekechea, shule za msingi hadi sekondari. Tunahitaji kuona watoto wote wa Busega wakienda shuleni.

"Niwasihi wazazi, fuatilieni mahudhurio ya watoto wenu ili kubaini kama kweli wanakwenda shuleni na wanasoma. Wanaporudi nyumbani, kagueni madaftari yao ili kuona wamejifunza nini. Zaidi ya hayo, wasimamieni watoto wa kike ili wahitimu masomo yao bila kubughudhiwa," amesisitiza.

Ni rai aliyotoa juzi wakati akizungumza na maelfu ya wajumbe waliohudhuria Mkutano Mkuu wa CCM wa Wilaya ya Busega uliofanyika kwenye viwanja vya Shule ya Sekondari Lion of Judah, wilayani Busega, mkoani Simiyu.

Waziri Mkuu alisema serikali imewekeza kwa kiwango kikubwa kwenye upatikanaji elimu nchini kwa kutoa fedha ya ujenzi wa shule, madarasa na mabweni.

"Rais ametoa fedha za elimu bila ada ili kuhakikisha kila mtoto wa kitanzania anapata fursa ya elimu," Waziri Mkuu Majaliwa alisema.

Kuhusu matumizi ya nishati safi ya kupikia, Waziri Mkuu alisema umefika wakati sasa taasisi zenye watu zaidi ya 100 zianze kutumia nishati hiyo huku akiwakumbusha wadau kuwa ukomo wa matumizi ya nishati chafu ni Desemba 31 mwaka huu.

"Wananchi mmoja waanze taratibu kuachana na matumizi ya nishati chafu kwa kubadilisha teknolojia. Tuhame kutoka kwenye kuni na mkaa na tuanze kutumia nishati ya gesi, umeme na aina nyingine ya mkaa ambao unatengenezwa kwa kutumia taka," aliagiza.

Majaliwa pia alitumia fursa hiyo kuwaelezea wajumbe wa mkutano huo, mafanikio yaliyofikiwa na serikali chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

"Fedha nyingi zimetolewa kwenye sekta ya elimu ambazo zimetumika kujenga miundombinu ya shule za msingi, sekondari na vyuo vya kati pamoja na ukarabati mkubwa wa vyuo vikuu," alisema.

Kwenye Sekta ya Afya, Waziri Mkuu alisema zimetolewa fedha nyingi kujenga vituo vya afya, hospitali za wilaya na za halmashauri zenye hadhi ya hospitali za wilaya pamoja na ujenzi wa hospitali za kanda.

Kuhusu umeme, Waziri Mkuu alisema: "Vijiji vyote vya mkoa huo vimepata umeme, imebakia tu kazi ya wananchi kuuvuta. Leo hii tunakwenda kwenye ngazi ya vitongoji na kupeleka umeme kwenye visiwa, iwe ni umeme wa jua au wa kupitisha kwenye bomba chini ya maji kwenda kwenye kisiwa kama cha Ukerewe."

Waziri Mkuu pia alisema utulivu uliopo kwenye Wilaya ya Busega unatokana na sera za CCM ambazo zinatabirika tangu enzi za waasisi wa taifa.

"Mshikamano na utulivu, kuwapo maadili ni utamaduni wa taifa letu na hata matokeo ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa yamedhihirisha imani waliyonayo wananchi kwa Chama Cha Mapinduzi," alisema.

Hata hivyo, kumekuwa na ukosoaji mkubwa kutoka kwa wadau wakiwamo viongozi wa dini na watetezi wa haki za binadamu dhidi ya uendeshaji wa uchaguzi huo.

Awali Mbunge wa Busega, Simon Songe alishukuru serikali kwa kuwezesha upatikanaji huduma nyingi za kijamii kwenye wilaya hiyo ndani ya muda mfupi.

"Watu wa Busega tuna imani sana na serikali ya awamu ya sita, maendeleo yaliyofanyika ni makubwa ukiwamo ujenzi wa reli ya kisasa. Tuna imani kuwa itakamilika mapema ili wakazi wa Busega waweze kwenda Dar es Salaam chini ya saa sita," alisema.

Pia alishukuru serikali kwa kutoa Sh. bilioni 19.9 ambazo katika kipindi cha Desemba 2020 hadi Oktoba 2024, zimewezesha utekelezaji miradi kadhaa ili kupunguza changamoto ya ukosefu wa vyumba vya madarasa, vyoo na madawati.

"Mradi wa VETA utakaogharimu Sh. bilioni 1.484 tayari umeshaanza kujengwa na ninaamini mwaka 2026 utakuwa umekamilika na wananchi wataanza kukitumia chuo hicho," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Kenan Kihongosi, alisema mkoa huo umepokea Sh. bilioni 858.5 ambazo zimetumika kuboresha sekta za elimu, afya, maji na umeme.

Alishukuru serikali kwa kupeleka magari ya wagonjwa manne, mradi wa maji kutoka Ziwa Victoria utakaogharimu Sh. bilioni 440 na ujenzi wa kituo cha kupozea umeme kwa gharama ya Sh. bilioni 97.

## KABWELA

FADHILI MOHAMED



# Wanawake washauriwa kuepuka mikopo kausha damu

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

WANAWAKE wameshauriwa kuacha kuchukua mikopo ya kausha damu ambayo inawadidimiza na badala yake wachangamkie mikopo inayotolewa na benki.

Meneja wa CRDB tawi la Chalinze, Exaud Mtui, amesema benki hiyo ina mpango mzuri wa kusaidia wanawake kupitia programu ya Imbeju ambapo kundi hilo linatakiwa kuichangamkia kujiinua kiuchumi.

Aliyasema hayo mwishoni mwa wiki mjini hapa wakati benki hiyo ilipokutanisha wanawake zaidi ya 200 kutoka vikundi vya wajasiriamali kwa ajili ya kuwapatia elimu ya mikopo na kusikiliza vikwazo vyao waweze kuvitafutia ufumbuzi.

Meneja huyo alisema programu hiyo ya Imbeju inamwezesha mwanamke kupata elimu ya usimamizi wa fedha na kupata mitaji isiyo na riba kwa ajili ya kuendeleza biashara zao.

"Epukeni mikopo inayowadidimiza, programu yetu ya Imbeju ni kwa ajili ya kuwainua wanawake itumieni kama fursa ya kuinuka kiuchumi, unganeni katika vikundi ambavyo vinalenga kuwakomboa kiuchumi," alisema Mtui.

Mbunge wa Chalinze, Ridhiwani Kikwete, alisema CRDB tawi la Chalinze ndio inayoongoza kwa makusanyo na kitendo chao cha kukutana na wanawake hao ni sehemu ya kurudisha kwa jamii.

"Rais amefungua milango kwa wawekezaji binafsi na hiki kinachofanywa na CRDB ni chakupongezwa kwani kupitia elimu na mikopo wanawake watafanya maendeleo na kuinuka kiuchumi kwenye jamii zao," alisema.

Ridhiwani ambaye ni Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Ajira na Vijana, alisema serikali itaendelea kushirikiana na wanawake kutatua vikwazo vinavyowakabili katika shughuli zao za ujasiriamali.

Naye Ofisa wa benki hiyo tawi la Chalinze, Boniphace Shija, aliwakumbusha wanawake kuepuka kuchukua mikopo umiza kwa kuwa kufanya hivyo hawawezi kuinuka badala yake wataendelea kudidimia.

Mmoja wa washiriki wa semina hiyo, Jenifa Moshi, mkazi wa Bwilingu kupitia kikundi chao walioomba benki kuwatembelea mara kwa mara kujua vikwazo vya wateja wao na kuzifanyia kazi kabla hazijaleta athari.

Pia, waliomba taasisi za kifedha kutoa mikopo kwa wakati ili wanawake wasiingie kwenye mikopo inayoumiza ambayo ina riba kubwa.



Mshtakiwa wa kesi ya kukutwa na kemikali, Iren Mseluka (kulia), akiwa chini ya ulinzi wa askari Magereza akielekea Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu Dar es Salaam jana kusomewa maelezo ya mashahidi katika kesi inayomkabili. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Wanafunzi UDOM waenda kujifunza vivutio utalii Iringa

**Zuhura Zukheri na Francis Godwin,** IRINGA

WANAFUNZI 300 wa kozi ya utalii na uhifadhi wa amali za jamii kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM) wamewasili mkoani hapa kwa ziara ya mafunzo ya siku tatu kujifunza vivutio vya kitalii na historia ya mkoa huo ili kuboresha uelewa kitaaluma.

Akizungumza jana wakati wa mapokezi ya wanafunzi hao, Mkurugenzi wa Jumba la Makumbusho la Iringa (Iringa Boma), ambaye pia ni Meneja wa Mradi wa Fahari Yetu, Jimson Sanga, alisema Mkoa wa Iringa una historia na vivutio vingi vya kipekee, ikiwa ni pamoja na Makumbusho ya Isimila, Kalenga kwa Mtwa Mkwawa, kaburi la Nyundo eneo la Lugalo, Hifadhi ya Wanyama ya Ruaha, na Maporomoko ya Udzungwa.

Sanga alisema kuwa Iringa ni moja ya mikoa yenye historia kubwa ya ukoloni na harakati za ukombozi wa Bara la Afrika.

Alisema jumba la makumbusho la Iringa limekuwa kivutio cha wageni wa ndani na nje wanaotaka kujifunza kuhusu historia ya mkoa huo.

"Ni matumaini yangu kuwa wanafunzi hawa hawatarudi UDOM wakiwa walivyoondoka, bali wakiwa wamebeba maarifa mengi yatakayowasaidia katika masomo na maisha yao ya baadaye," alisema Sanga.

Mwalimu wa utalii na uhifadhi wa amali za jamii kutoka UDOM, Selina Banzi, alieleza kuwa ziara hiyo inalenga kuwasaidia wanafunzi kuelewa masomo kwa vitendo. Aliongeza kuwa walimu waliona Iringa kuwa mahali sahihi kwa mafunzo hayo kutokana na utajiri wa vivutio na historia yake.

"Ziara hii imewapa wanafunzi nafasi ya kujifunza kwa vitendo, na pia imepunguza maswali yao darasani. Tunawashukuru Iringa Boma kwa ukarimu wao na usaidizi mkubwa waliotupatia," alisema Banzi.

Wanafunzi walieleza kufurahishwa na fursa ya kujifunza kuhusu vita vya Wahehe dhidi ya Wajerumani, uongozi wa Mtwa Mkwawa na umuhimu wa eneo la Lugalo. Walitembelea kaburi la Nyundo, ambalo lina historia ya wapiganaji waliopoteza maisha katika vita hiyo.

Walisema kuwa ziara hiyo imewawezesha kuelewa vyanzo vya majina ya maeneo kama shule za Lugalo na kambi ya Jeshi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ) Lugalo, ambazo zina asili kutoka eneo la Lugalo mkoani Iringa.

## NHIF yataka kupelekewa madai mapema

**Na Steven William,** MUHEZA

WAGANGA wafawidhi wa zahanati, vituo vya afya na hospitali Wilaya ya Muheza wametakiwa kujenga utamaduni wa kupeleka madai yao mapema katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) ili kupata malipo yao.

Ofisa udhibiti ubora mwandamizi kutoka Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya Mkoa wa Tanga, Emmanuel Bilikundi, alisema hayo alipokuwa akitoa mafunzo kwa waganga hao katika kikao cha maandalizi ya mpango kabambe wa afya kwa mwaka wa 2025/2026 kilichohudhuriwa na Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Muheza, Issa Msumari.

Aliwataka waganga kujenga utamaduni kudai malipo kwa wakati NHIF ili kuendelea kuboresha huduma ya matibabu kwa wananchi kwa uhakika.

Bilikundi alisema sasa NHIF wameboresha mfumo wa malipo kwa muda wa siku 45 wanapoandikiwa madeni na vituo vinavyotolea huduma ya afya.

Aidha, alisema ugonjwa wa figo, kisukari na magonjwa mengine yasiyokuwa ya kuambukiza yameongezeka kutokana na watu kutofanya mazoezi na zaidi ya asilimia 50 ya malipo ya NHIF yanakwenda katika magonjwa hayo.

Aliwataka watumishi na wananchi kuhakikishe wanajikita kufanya mazoezi kupunguza magonjwa hayo na kwamba NIHF itasapoti kila Kumamosi ya mwisho wa mwezi mazoezi hayo pamoja na kupima ugonjwa wa kisukari.

Ofisa Madai Mwandamizi kutoka NHIF Mkoa wa Tanga, Petro Aloyce, alisema NHIF imejipanga kulipa madeni yote kwa wakati katika vituo vya afya, zahanati na hospitali.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Muheza, Dk. Fani Mussa, alisema wanaendelea kuboresha huduma za afya katika wilaya hiyo kwa kuongeza ukusanyaji wa mapato katika zahanati, vituo vya afya na hospital ya wilaya ili kununua dawa kwa wingi kutoka MSD ili wananchi wapate huduma bora.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Muheza, Issa Msumari, alisema kumekuwa na tabia serikali kuleta fedha katika sekta ya afya kwenye vituo, lakini hazitumiki mpaka mwaka unapita halafu zinarejeshwa tena serikali kuu.

# TFS kuwaondoa wavamizi wa misitu

**Na Hamida Kamchalla,** TANGA

WAKALA wa Huduma za Misitu (TFS) Kanda ya Kaskazini itaanza kutekeleza agizo la serikali kuwaondoa wananchi, wakiwamo kijiji kizima kwa kuvamia misitu, kujenga makazi na kufanya shughuli za kilimo.

Akizungumza katika kikao cha pamoja na wadau wa uhifadhi, Meneja wa TFS wa Kanda hiyo, Kamishna Mwandamizi wa Uhifadhi, James Nshale, alisema serikali kupitia vikao vya wilaya imeagiza wavamizi wote waondolewe kwenye maeneo ya hifadhi.

Alitaja maeneo hayo kuwa ni Hifadhi ya Chang'andu iliyopo Wilaya ya Korogwe kwa ajili ya kuhifadhi miti asilia, Hifadhi ya Gendagenda iliyopo Wilaya za Pangani na Handeni ambako kijiji chote cha Kwabojo kinatakiwa kuhamishwa ili kulinda hifadhi hiyo.

Alisema Hifadhi ya Bondo, wananchi kutoka Manyara, wamevamia ardhi yenye ukubwa wa hekta 18,000.

Katika hifadhi hiyo, wananchi zaidi ya 2,000 wa kabila la Wambulu wanaishi humo wakifanya shughuli za kilimo na ufugaji.


Vilevile, wananchi hao wamejenga makazi, makanisa na shule ya msingi iliyojengwa kwa fedha za COVID 19.

"Tumeanza mchakato wa kuwaondoa watu hifadhini ili kulinda misitu hiyo kwa vizazi vijavyo, tukisema tuwaache tuhalalishe vijiji vyao maana yake itakuwa siyo nchi watu watavamia hifadhi na kufanya makazi wakijua wataachwa na mamlaka, hii haikubaliki lazima watoke," alisema.

Alisema TFS Kaskazini, ina hifadhi za misitu asilimia tano ambazo Amani, Nilo, Magamba zilizopo mkoani Tanga, Chome iliyopo Same (Kilimanjaro) na Ismangoli (Arusha).

Mkuu wa Wilaya ya Korogwe, William Mwakilema, alisema Mkoa wa Tanga upo tayari kulinda na kuendeleza rasilimali za hifadhi zote za misitu na wale wote waliovamia wataondolewa kwa kufuata sheria.

Mwakilema, aliwataka TFS kuhakikisha wanapanda miti katika maeneo ya uhifadhi ikiwamo ya mianzi (Bamboo) kwa ajili ya kutengeneza samani.




Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Muheza, mkoani Tanga, Issa Msumari (kulia), akisalimiana na Mratibu wa Ukimwi, Mohamed Juma (kushoto), kabla ya kuingia katika kikao cha maandalizi ya mpango kabambe wa afya kwa mwaka 2025/26 juzi. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Wenyeviti watangaza vita unyanyasaji kingono

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

VIONGOZI zaidi ya 40 wa Serikali za Mitaa wilayani hapa Mkoa wa Kilimanjaro wameapa kwa siku 100 za utawala wao kukabiliana na changamoto za unyanyasaji wa kingono katika maeneo yao.

Unyanyasaji huo ni ule unaofanywa dhidi ya wanafunzi wa vyuo vikuu na wasichana wenye umri mdogo, ambao hawajajitambua wala kukomaa kifikra.

Mjumbe wa Serikali ya Mtaa wa Mwereni, Kata ya Mfumuni, Manispaa ya Moshi, Catherine Kusaga, alisema wengi wa wanavyuo wanaofanyiwa ukatili wa kingono ni wale wanaoishi nje ya chuo.

Kusaga na wenzake, waliahidi kushughulikia changamoto hiyo mwishoni mwa wiki iliyopita wakati wa warsha ya kuwajengea uwezo wenyeviti wa mitaa na wajumbe wao iliyoandaliwa na Shirika la kiraia la KWIECO kupitia Mradi wa Sauti ya Haki unaofadhiliwa na Women Fund Tanzania Trust (WFT).

"Unakuta hao wanafunzi wanapanga chumba wanaishi katika mazingira ambayo siyo sahihi, wanakaa wengi chumba kimoja na wengi wanafunga ndoa zisizo halali," alisema na kuongeza kuwa:

"Wanafunga ndoa za utotoni, wanajihalalisha wenyewe huo ni udhalilishaji wa kingono na pia inaadhiri jamii hasa wazazi wa watoto wale, kumbe watoto wameshafunga ndoa haramu na wameshapata mimba na wengine watoto."

Mwenyekiti wa Serikali ya Mtaa wa Matindigani Kata ya Pasua, Amos Chimachibago, alisema baada ya kupatiwa mafunzo, wanarudi kwenye jamii kwenda kutoa elimu kwa wazazi jinsi ya kuwawezesha watoto wao kifedha na kuondokana na udhalilishaji vyuoni.

"Baada ya kupigwa msasa sasa tunaenda kutoa elimu kwa wazazi wanaopeleka watoto wao vyuo wawe na uhakika wa mahali wanapoishi watoto wao, kuwafuatilia, kuwawezesha kifedha kama hawajapata mkopo wa vyuo vya elimu ya juu," alisema.

Alisema aliokota kichanga kimetupwa jalalani, aliumia sana na kupatwa na huruma, hivyo anachokifikiri katika uongozi wake ni kupambania kutoa elimu kwa wananchi.

Mratibu wa Mradi wa Sauti ya Haki, Veronica Ollomi, alisema katika warsha hiyo walikuwa wanakumbushana wajibu kama viongozi baada ya kuingia madarakani kusimamia haki kwa jamii na kutokomeza ukatili wa kijinsia katika maeneo yao.

Kuhusu udhalilishaji wa kingono, alisema vyuo vingi viwe vya kati au vyuo vikuu, watoto wa kike wanakumbana na vitendo hivyo.

"Kwa hiyo wanapokuja katika vyuo wanajifunza maisha mapya ambayo hakuwahi kuwa nayo walikotoka na zile tabia mpya wanazojifunza ndio zinasababishia wakati mwingine kukutana na changamoto ya udhalilishaji wa kingono," alisema Mratibu huyo.

# Uoto wa asili upo hatarini kutoweka

**Na Oscar Assenga,** TANGA

HEKTA zaidi ya 462,000 za misitu zinaharibiwa kila mwaka nchini kwa uvunaji haramu miti na uchomaji moto na kupoteza uoto wa asili.

Mtaalamu wa Hifadhi wa Wizara ya Masiliasili na Utalii, Dk. Sima Makengesa, aliyasema hayo wakati wa kikao cha wadau wa misitu kilichoandaliwa na Taasisi ya Can Tanzania.

Makengesa, ambaye ni Mtaalamu wa Misitu na Nyuki, alisema Wizara ya Maliasili na Utalii ipo kwenye mikakati ya kuwasaidia wananchi kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

"Kama nchi tumejiwekea malengo, tutarejesha hekta milioni 5.2 ifikapo 2030, na kwenye mkutano huu tupo kuangalia mikakati ya kurejesha asili ya maeneo yetu yaendelea kuwa salama na kuwasaidia kuwa na mvua za kutosha," alisema.

Alisema nchi imeweka azimio la kufikia lengo la kupunguza gesi joto na kuleta mabadiliko ya tabia ya nchi kufikia mwaka 2030 kwa kupunguza uzalishaji wake kwa asilimia 30.

Alisema gesi joto hizo zinaletwa na kazi za binadamu kwa kilimo, kuchoma misitu na matumizi ya nishati.

Alisema juhudi za Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, kinara wa kuleta nishati safi nchini ni chachu ya kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi.

Alisema kwa sasa katika Sekta ya Misitu na Nyuki, wanatunga sera, kanuni na mwongozo ili kuwasaidia wananchi kutunza mazingira yao, misitu ya vijiji na misitu binafsi na kuepuka uvamizi kwenye misitu ya serikali kuu.

Aliwataka kushirikiana kufanya kazi ili kulinda rasilmali za misitu ili kukabiliana na mabadiliko ya tabia ya nchi yanayotokea nchini.

"Hakuna sheria yoyote inayotoa ruhusa ya kuharibu mazingira na sheria zao zote na taratibu na kulinda mazingira," alisema.

Dk. Sima alisema wataendelea kushirikiana kulinda rasilimali misitu kwa ajili ya kuinua uchumi na wananchi wanapata faida.

Awali Ofisa Misitu Mkuu wa Wakala wa Hifadhi za Misitu Tanzania (TFS), Maria Kapina, alisema wamekuja na njia mbadala kufanya uhifadhi uendelevu misitu kwa kuhusisha jamii.

Kapina, alisema wanatumia teknolojia ya kutumia picha za anga kuchakata ili kujua misitu iliyoharibiwa vibaya na iliyohifadhiwa.


"Kwa ile ambayo imeharibiwa tunafanya upandaji mara ya pili kwa misitu asili na mashamba pia tukikutana eneo limeharibika sana na mwingilio wa binadamu ni mdogo wanalifunga na kuzuia shughuli za kibinadamu kufanyika," alisema.

Awali Mratibu wa Mradi kutoka Taasisi ya Can Tanzania, Sharon Kishenyi, alisema upande wa Pangani mradi huo unatekelezwa kwenye vijiji vya Msaraza na Mpakani na kurejesha mikoko kukabiliana na mabadiliko ya nchi.

Sharon, alisema mradi huo unatekelezwa katika Kijiji cha Kigurusimba kwa ajili ya kuhifadhi msitu wa Kwasinge.

Alisema katika Kijiji cha Msaraza wamepanda miti takribani 24,000 na kwamba wanaendelea na mradi huo wilayani Same Mkoa wa Kilimanjaro kwenye kijiji cha Vumari.

Sharon, alisema kijijini hapo kuna msitu wenye manufaa makubwa kwa kuchangia upatikanaji wa maji kwa jamii hasa katika mji wa Same.





# Polisi ahukumiwa kifungo kwa mauaji

**Na Ambrose Wantaigwa,**
MARA

ASKARI wa Kituo cha Polisi Sirari Wilaya ya Tarime, Kululetela Samwel, amehukumiwa kifungo cha mwaka mmoja nje kwa kosa la kumuua bila kukusudia Ng'ondi Masiaga kwa kumpiga risasi wakati wakizuia kwenye mpaka wa Sirari.

Hukumu hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki iliyopita na Jaji Kamazima Kafanabo katika Mahakama Kuu Kanda ya Musoma baada ya mshtakiwa huyo kupatikana na hatia ya mauaji hayo wakati mshtakiwa huyo na askari mwenzake wakifanya doria ya kuzuia uvushaji wa bidhaa kinyume na sheria kwenye mpaka huo wa Tanzania na Kenya.

Kwa mujibu wa taarifa ya hukumu hiyo, iliyotolewa na Mwendesha Mashtaka upande wa Jamhuri, Davis Katesigwa, mshtakiwa huyo alitenda kosa hilo Machi 31, mwaka jana katika Kijiji cha Kubiterere Wilaya ya Tarime mkoani hapa.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa huyo na askari mwenzake, kila mmoja alikuwa na bunduki kwenye doria hiyo wakisaidiana na maofisa wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) wakuzia uvushwaji wa bidhaa kwa njia ya magendo katika nchi hizo.

Ilidaiwa kuwa mshtakiwa huyo na askari mwenzake, walianza doria katika mpaka huo kabla ya maofisa hao wa TRA kufika kinyume na maagizo yaliyotolewa.

Katesigwa alidai wakati askari hao wakiwa katika doria hiyo, waliwakamata watu waliokuwa wakisafirisha saruji kwa njia ya magendo kwenye mpaka huo kwa kutumia pikipiki, akiwamo Masiaga aliyekuwa akitumia aina ya Honlg yenye namba za usajili MC 577 CZF.

Alidai wakati wa kuwakamata watuhumiwa hao, inadaiwa yalitokea mabishano kati ya Masiaga na mshtakiwa huyo kuruhusu kushikiria pikipiki hiyo na bidhaa za magendo.

Katasigwa alidai wakati Masiaga akilazimisha kuondoa pikipiki yake, mshtakiwa huyo alimpiga risasi mbili, moja kwenye nyonga na nyingine pajani na kusababishia kuvuja damu nyingi.

Alidai Masiaga alifariki dunia katika Hospitali ya Wilaya Tarime wakati akipatiwa matibabu.

Baada ya kifo hicho kutokea, mshtakiwa huyo alikamatwa na kuwekwa mahabusu kisha kufikishwa mahakamani kujibu mashtaka hayo ya mauaji, akitetewa na Wakili David Juma.

Katika kesi hiyo, Jamhuri iliwasilisha mahakamani mashahidi saba ambao walithibitisha mauaji hayo kwa kutoa vielelezo 15. Kwa upande wa mshtakiwa, alikuwa na mashahidi wanne na vielelezo viwili.

Baada ya kusikiliza pande zote mbili, Jaji Kafanabo, alisema mahakama hiyo inamtia hatiai mshtakiwa huyo kwa kuua bila kukusudia kinyume na kifungu cha 195 cha sheria ya kanuni ya adhabu namba 16 iliyofanyiwa marejeo 2022.

"Kwa hiyo mahakama hii inamhukumu mshtakiwa kutumikia kifungo cha nje kwa muda wa miezi 12 kwa masharti kuwa hatatenda kosa katika kipindi hicho," alisema.

## Wanaonyemelea majimbo, kata CCM kufyekwa

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Shinyanga kimeonya kitafyeka majina ya wanachama wanaopita kwenye majimbo kusaka ubunge na udiwani kabla ya wakati kwa kutengeneza makundi na kuzua hofu kwa viongozi waliopo.

Onyo hilo lilitolewa na Mwenyekiti wa CCM wa Mkoa huo, Mabala Mlolwa kwenye Mkutano Mkuu wa Jimbo la Ushetu uliofanyika mwishoni mwa wiki iliyopita.

Mlolwa, alisema chama hicho kina taarifa ya kila mwanachama anayejipitisha kwenye majimbo na kata na ushahidi wa video zinazoonyesha yale wanayoyafanya.

"Mnaopita majimboni kabla ya muda mnatuvurugia chama na kuwatia hofu wabunge na madiwani wetu waliopo wanashindwa kufanyakazi zao vema," alisema na kusisitiza kuwa: "Mnatengeneza makundi ya kuwatafutia kura na kutumika kugawa vijizawadi kwa wanachama na wananchi. Sasa nitawapitia na upanga wa shetani bila huruma."

Aliwataka makatibu wa matawi, kata na vitongoji wa chama hicho kuendelea kutoa taarifa za wagombea wanaojitokeza kutafuta kura kabla ya wakati kwa kuwasilisha ushahidi wa sauti, picha na picha mjongeo ili kutumika katika maamuzi.

Mkuu wa Wilaya ya Kahama, Mboni Mhita, alisema wabunge na madiwani waliopo wanatekeleza majukumu yao vizuri na kuwapelekea wananchi maendeleo katika sekta ya afya, elimu, kilimo na miundombinu ya barabara, lakini wanakwamishwa na wanachama wanaojipitisha na kuunda makundi ya kuwatafutia kura na kuwafitinisha kabla ya chama hicho kuwateua baada ya waliopo kumaliza muda wao.

Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Cherehani, alisema kwa kipindi cha kuanzia mwaka 2021 mpaka 2024, walipokea Sh.bilioni 190 na kutekeleza miradi ya maendeleo katika sekta ya afya, elimu, kilimo, nishati, barabara, maji pamoja na mifugo.



Ofisa Maendeleo ya Jamii Kata ya Mtendaji, Halmashauri ya Tabora Mjini, mkoani Tabora, Paskalina Sulle, akizungumza kwenye hafla ya kugawa bima za afya kwa kaya zenye watu walio na ulemavu wa akili mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# RC ahadharisha Ukimwi, akemea *Single Mother*

**Na Marco Maduhu,**
SHINYANGA

MKUU wa Mkoa wa Shinyanga Anamringi Macha, amewataka wananchi kujihadhari na maambukizi ya Virusi vya Ukimwi kutokana na takwimu kuonyesha yameongezeka kwa asilimia 5.6 mkoani hapa huku ya kitaifa yakiwa asilimia 5.1.

Macha alitoa takwimu hizo juzi wakati Shirika la FHI 360 kupitia Mradi wa EPIC, likikabidhi vifaa vya kujikwamua kiuchumi kwa mabinti ambao ni wanufaika wa mradi huo na makabati 15 ya kuhifadhi nyaraka katika vituo vya afya vya halmashauri tatu za mkoa huo.

Mradi huo, umelenga kupunguza maambukizi mapya ya Virusi Vya Ukimwi (VVU) kwa mabinti wenye umri wa kuanzia miaka 15 hadi 24 ambao wapo nje ya shule.

Macha aliwataka wakazi wa mkoa huo kujenga utamaduni wa kupima VVU ili kujua afya zao na kama wamepata maambukizi hayo waanze kutumia dawa za kufubaza virusi hivyo.

Alisema mpaka sasa takwimu zinaonyesha kuwa mkoa huo una watu 72,000 wanaotumia dawa hizo na kuwataka wakazi hao kuwa makini na ngono zembe.

Katika hatua nyingine, Mkuu huyo wa mkoa, amekemea tabia ya baadhi ya wanawake wanaoishi bila wanaume na kulea watoto peke yao kwa kuwa wanawanyima watoto hao haki ya kuwatambua baba na kutaja kitendo hicho kuwa ni moja ya ukatili wa mtoto.

**Macha alitoa takwimu hizo juzi wakati Shirika la FHI 360 kupitia Mradi wa EPIC, likikabidhi vifaa vya kujikwamua kiuchumi kwa mabinti ambao ni wanufaika wa mradi huo na makabati 15 ya kuhifadhi nyaraka katika vituo vya afya vya halmashauri tatu za mkoa huo.**

Alisema wanawake hao wanapenda kuwa na mahusiano na wanaume mbalimbali, kisha kuzaa watoto na kuanza kuishi bila wanaume wakijiita 'Single Mother' hali aliyoitaja ni kuhatarisha mstakhbari wa watoto hao na kuwaingiza wazazi kwenye hatari ya maambukizi ya Virusi Vya Ukimwi (VVU).

Kaimu Mganga Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Dk. Faustine Mlyutu, alisema hafla hiyo ni mwendelezo wa shughuli za wadau wao katika mapambano dhidi ya VVU.

Dk. Miyutu, alisema walianza kutoa elimu kwa mabinti kujikinga na maambukizi mapya ya VVU na sasa wanawapatia vitendea kazi ili wajikwamue kiuchumi.

Kaimu Meneja wa EPIC, Getrude Eusebio kutoka FHI 360, alisema kupitia mradi huo ulioanza mwaka 2020 hadi sasa wamewapatia mabinti hao vyerehani, majora ya vitambaa, vifaa vya saloon, kompyuta na print ili wajiajiri, kuepuka maisha hatarishi na maambukizi mapya ya VVU..

Nipashe
# TESA
Jumanne Desemba 24, 2024
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI

Ukurasa 12



Ndivyo yanavyoibuka maajabu mapya bonde la Mto Congo

Ukurasa 13



Teknolojia ya kisasa itakavyoipaisha chai

Ukurasa 14



Raha ya barabara nzuri Dar inapogeuka karaha ya usafiri

NA MWANDISHI WETU

DIRA 2050

# Bado inakosa majibu kuinua wanawake sekta isiyo rasmi

TAIFA lisilo na dira ni kama taifa bila roho. Lakini pia kuwa na dira isiyozingatia usawa wa kijinsia na kuhakikisha maendeleo ya wanawake na makundi maalumu ni kuwa na nchi japo ina roho lakini iko mahututi.

Ndiyo haja ya dira kuwagusa wanawake kwa sababu ni nguvu kazi na injini ya maendeleo ya karibu sekta zote. Mfano ndiyo wanunuzi wa bidhaa za viwandani za vyakula, mavazi na dawa japo kazi zao ziko kwenye sekta isiyo rasmi.

Kwa kuliona hilo, wanamtandao wa wanawake na dira, wanahakiki Dira ya Maendeleo ya Taifa ya 2050, wakisema ni lazima dira hiyo iunganishe na kutambua uwepo na ushirikiano wa sekta isiyo rasmi iliyosheheni wafanyabiashara wanawake na sekta binafsi ili kufikia uchumi shindani na endelevu.



Jane Magigita na Profesa Ruth Meena (kulia), wakitoa maoni ya wanamtandao wa wanawake na dira kwa viongozi wa Tume ya Mipango. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

Mjumbe wa wanamtandao, Jane Magigita, anagusa kipengele cha dira kinachozungumzia kuwapo uchumi jumuishi, tulivu na unaotabirika, katika mkutano na Tume ya Mipango inayoandaa dira hiyo.

Anasema wanawake wanachotaka ni kuona taifa lenye uchumi jumuishi na linganifu na sera za uchumi zitakazowawezesha kunufaika na fursa zote za kiuchumi zilizoko.

Ni fursa za kibiashara, uwekezaji, huduma za kifedha, matumizi ya teknolojia yenye tija.

Aidha, wanamtandao wanataka kuwe na mikakati ya makusudi ya kuwekeza kwenye sekta zinazotoa ajira na kumgusa mwanamke moja kwa moja kama kilimo, madini, afya, elimu na mfumo mzima wa upatikanaji wa kazi na shughuli halali za kuongeza na kupata kipato zinazowagusa wanawake.

**SEKTA ISIYORASMI**

Wanawake na dira wanasema sekta binafsi imefafanuliwa kikamilifu lakini kunakosekana muunganiko (dislink) kati yake na ile isiyo rasmi.

"Kwenye 'private sector dialogue' au kongamano la kitaifa la serikali na sekta binafsi linakosekana kundi hili muhimu la sekta isiyo rasmi. Halichukuliwa kama sehemu ya sekta binafsi, kuna 'dis-linki' kati ya sekta hizi. Tunataka dira iziunganishe."

Jane anaueleza ujumbe unaoongozwa na Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Mipango na Uwekezaji, Stanslaus Nyongo, kuwa mikutano hiyo haiishirikishi sekta isiyo rasmi. Inaachwa kama vile siyo kundi muhimu linalochochoea injini ya maendeleo ya sekta binafsi rasmi.

"Mfano ni mamalishe ndiyo wanunuzi wakuu wa mafuta ya kula yanayozalishwa na viwanda ambavyo ndivyo sekta binafsi rasmi, naweza kusema ndio wanaovishika kiuchumi. Ni wapishi wakubwa wanaolisha mamilioni mijini, majiji na vijijini." Anasema Jane.

Anafafanua kuwa kwenye maendeleo ya uchumi na mnyororo mzima wa thamani wa mafuta ya kula wanawake hao ni watumiaji wakubwa zaidi wa bidhaa hiyo na ndiyo wanaochochea kukua viwanda hivyo lakini dira haikuwagusa, kwa maana ya sekta isiyo rasmi.

Anasema hata kama ni wanunuzi wadogo lakini uwingi wao unafanya kuwa wateja wakubwa wa bidhaa hiyo, japo kundi hilo linasahaulika.

Anasema yanapozungumziwa mazingira wezeshi kuondoa kodi na ada zinazokwamisha biashara na uwekezaji hakuna mfanyabiashara wa sekta isiyorasmi anayezungumziwa ni wafanyabiashara wakubwa.

Anakumbusha kuwa ni lazima dira iwatambue na iwaingize kwenye sera za kujenga uchumi shindani kwa kuwa wanawake hao ndiyo wanaotoa kodi za halmashauri, kodi za serikali, ndiyo wanatumia huduma za kijamii kama maji, barabara, vyoo, kumbi na kulipa kodi na tozo na kuendesha uchumi wa nchi.

Wanawake wanataka dira itamke maana ya uchumi juimuishi na mfumo wa uchumi, jumuishi na linganifu na kuwe na maelezo ya matarajio ambayo yatapimwa kuangalia matokeo na mafanikio.

**TABIANCHI**

Mariya Matuja, anazungumzia suala la usawa wa kijinsia kuwa halijajitokeza kikamilifu kwenye dira ya maendeleo 2050, kwenye kukabiliana na athari ya mabadiliko ya tabianchi na kujenga uhimilivu.

Anakumbusha kuweka masuala ya kijinsia na mabadiliko ya tabia ili kujua ni kiasi gani wanawake wanaathirika na matokeo ya mabadiliko hayo.

Lakini pia kufahamu ni kwa vipi mtoto wa kike anaathirika na tunafikiria kuwa ifikapo 2050 yatakuwa yamefikia hali gani na ni kwa namna zipo wanawake watakuwa wanayakabili na kuyahimili.

Maria anazungumzia biashara ya kabon, akisema kwenye kipengele cha mabadiliko ya tabianchi dira haijamzunguzia mwanamke na kwenye miongozo haimgusi mwanamke.

"Kama kwenye miongozo haijawekwa ni wapi atazungumzwa?" anahoji Mariya.

Anakumbusha kuwa tabia nchi inahusu ardhi, rasilimali na umiliki wake. Lakini kama mwanamke anawekwa pembeni na walio wengi hawamiliki aradhi itakuwa vigumu kuhimili.

Anawashauri wajumbe wa dira kuangalia kila kipengele kuhusu uhimilivu na masuala yote yaangalie wanawake wataathirikaje na washiriki kutatua changamoto.

"Tunatamani kuona matarajio ambayo yameongelewa kwenye mabadiliko ya tabia nchi na ardhi suala la jinsia lionekane, lieezeke na lifahamike. Sote tunafahamu mabadiliko ya tabianchi ni nini, lakini je, tumeiandaa Tanzania kiasi gani? Kizazi chetu cha sasa tumekiandaaje na masuala ya sayansi na teknolojia tumeyaingizaje kukabiliana nayo? Ni kwa kiasi gani ni sehemu ya mabadiliko ya tabia? Mwanamke yuko sehemu gani?

**MADINI**

Profesa Ruth Meena, katika mkutano wa kuhakiki dira, anazungumzia madini, akisema dira haijawagusa wachimbaji wadogo ili

INAENDELEA UK. 12

SAYANSI

NA MWANDISHI WETU

# Ndivyo yanavyoibuka maajabu mapya bonde la Mto Congo



Mamba mdogo aliyegunduliwa ndani ya bonde la Mto Congo mwaka 2018. **PICHA: BBC**

BONDE la Mto Congo maarufu 'mapafu ya Afrika' ikimaanisha kuwa limesheheni misitu minene inayofyonza hewa ya kabon na kuachilia oksijen, linaendelea kuwa makazi ya viumbe wanaofahamika na wapya wanaogundulika zama hizi.

Eneo hilo linategemewa na dunia kupunguza makali ya mabadiliko ya tabianchi yanayoongeza joto duniani.

Mkuu wa Uhifadhi wa Bonde la Congo, Jeap Van Der Waarde, anasema asilimia 78 ya viumbe na utajiri vilivyomo ndani ya msitu huo havijulikani.

Der Waarde anaeleza kuwa mbali na kuwa na viumbe hai wengi wa kipekee, bonde hilo ndilo linalofanyakazi wakati huu ya kusafisha hewa duniani, kati ya safu za misitu ya mvua duniani, tofauti na msitu wa Amazon, ambao umekuwa ukipoteza uwezo huo.

"Spishi mpya zinaweza kulindwa iwapo zitaendelezwa. Tusisahau kwamba bonde la Congo linahitaji sana utulivu wa hali ya hewa," anasema der Waarde.

Katika ripoti ya Shirika la Uhifadhi wa Wanyamapori (WWF) iliyotolewa hivi karibuni, imeeleza kuwa licha ya utajiri uliohifadhiwa katika misitu ya Congo, kuna viumbe vingi vipya vinavyoishi ambavyo dunia havifahamu.

Katika ripoti hiyo inaeleza ndani ya misitu ya Congo kuna bundi mwenye tabia za kipekee ambaye sauti yake inafanana na paka.

Bundi wa nchini Principe, aliyegunduliwa mnamo 2022, hupatikana katika taifa dogo la kisiwa cha Sao Tomé na Príncipe.

Kichwa chake kimepambwa na masikio yenye muundo wa tawi. Kwa mujibu wa Jarida la Birds of the World, ambalo linahifadhi data ya ndege duniani, bundi huyo yuko hatarini kutoweka kutokana na kuishi katika mazingira yenye idadi ya watu kati ya 1,100 hadi 1,600.

### KERENG'ENDE WA PINKI

Nchini Uingereza wanafahamika sana kereng'ende wa rangi ya pinki tangu walipoonekana katika miaka ya 1970. Hata hivyo, mdudu huyo jamii ya panzi anayeruka kwa kutumia mbawa zake amezidi kuwa maarufu baada ya kubaini kuwa wapo kwa wingi kwenye bonde la Congo.

Timu ya wanasayansi ambao hawakupinga walipomuona mdudu huyo, wanakubaliana kwamba ni kereng'ende anayepatikana Ulaya.

### NYOKA HATARI

Licha ya kugunduliwa tangu 2020, nyoka 'mongo' anayesifika kwa na sumu kali na ngozi inayoota nywele, akijulikana pia kuwa miongoni mwa aina ya nyoka hatari zaidi Afrika anaishi Congo.

Mongo ni nyoka hatari zaidi hasa kutokana na uwezo wake wa kubadilika rangi anapotafuta mawindo lakini pia mchanganyiko wa rangi ya kijani, njano na nyeusi inamruhusu nyoka huyo kutogundulika kwa urahisi katika mazingira ya misitu.

### CHURA MDOGO

Ndani ya misitu ya Congo, kuna chura wa Congo ambao hadi sasa wanaonekana katika katika eneo hilo pekee kusini mwa Mto Congo.

Wanaelezwa kuwa ana urefu usiofikia sentimita nne na kuishi kwake katika eneo dogo, hutumika kama kiashiria muhimu katika mabadiliko ya hali ya hewa kwenye makazi yake.

Ukubwa wa bonde la mto Congo ni hekari 500, ambazo ni sawa na kilomita za mraba milioni 3.4. Eneo lake linakaribiana na ukubwa ukiziunganisha pamoja Tanzania, Kenya, Uganda, Burindi, Rwanda na Somalia.

Bonde la Congo lina misitu minene yenye mimea ya kila aina na inashika nafasi ya pili badala ya msitu wa Amazon ulioko Amerika Kusini.

Bonde la Mto Congo limesambaa kuanzia Congo yenyewe, Cameroon, Jamhuri ya Afrika ya Kati, Jamhuri ya Congo, Equatorial Guinea na Gabon.

WWF inaeleza kwamba zaidi ya aina 700 za wanyamapori na mimea zimegunduliwa na wanasayansi ndani ya Bonde la Kongo katika kipindi cha miaka 10 iliyopita.

Kutokana na ukubwa wake wa eneo miti mikubwa iliyoshikana, bonde la Congo linashikilia nafasi ya pili kwa kusababisha mvua duniani.

Pia ni eneo kubwa lenye kisima kikubwa zaidi cha kuvuna hewa ya kaboni duniani kuliko ile inayotolewa.

Ripoti hiyo inaeleza jinsi wanasayansi duniani kote wanavyokubaliana kwamba msitu huo kama bayoanuai ya ajabu ambayo inahitaji kuhifadhiwa ili kuendelea kuendesha mifumo muhimu ya maisha ya viumbe hai na ikolojia duniani.

Mwezi uliopita, WWF ilichapisha matokeo ya hifadhi za dunia za asili ambazo zilionyesha kupungua kwa asilimia 73 kwa idadi ya wanyamapori duniani.

# BADO INAKOSA MAJIBU KUINUA WANAWAKE SEKTA ISIYO RASMI

INATOKA UK.11

kuwa wamiliki wa migodi hasa wanawake.

Aidha, haijaingizwa namna mwanamke atakavyofaidika na kuepushwa na unyanyasaji wa kijinsia kwenye sekta ya migodi.

"Tunataka dira iwaguse wachimbaji wadogo na pia wanawake watazamwe kwa jicho la kipekee, walindwe na kuhakikishiwa huduma za ziada ili wasiwe kwenye unyanyasaji migodini."

Wapate huduma kama zana bora za kuchimba na kuchenjua lakini pia waangaliwe na usalama wao kijinsia kwenye sekta hiyo ambayo pia inakua kwa kasi, anasema Profesa Ruth.

### UCHUMI BLUU

Ni jambo linalotakiwa lifafanuliwe kwa wananchi kwa kuwaeleza na kuwapatia ufahamu zaidi wa nini maana ya uchumi wa bluu, anasema Ruth.

Pamoja na uchumi wa bluu anataja biashara ya karbon ambayo anasema mtandao wao unazo tafiti kuwa watu wengi hawaifahamu karibu kote vijijini na mijini.

"Vijijini watu wamedanganywa na kuachilia hati miliki za mashamba yao ya miti kwenye biashara ya kaboni hii ni dhana ngeni. Tunapendekeza kuwapo na kampeni za kuitambulisha na kuujulisha umma."

Anasema wanatoa hati miliki za mashamba yao kwa wageni lakini hawafahamu kwa uhalisi nini biashara hiyo na hata faida wanayopata.

Anaongeza kuwa kutokana na kukosa ujuzi na utaalamu wajanja wamechukulia ujinga wa wananchi kama fursa ya kujineemesha na kufaidika, hayo mambo yazungumzwe na dira yasifanyike bila wananchi kupata uelewa na elimu ya kutosha.

Ili kufanya biashara ya kabon inabidi wakulima wawe na mashamba yenye ukubwa fulani ambayo yana miti yenye uwezo wa kuzalisha oksijeni ili mgeni au mwekezaji anunue oksjeni hiyo kulinda na ile inayozalishwa Ulaya au Marekani.

Hata hivyo, wananchi hawafahamu utaalamu huo wala namna ya kupima oksjeni inayozalishwa, kupata gharama halisi wanayohitaji kulipwa.

Mambo hayo hufanywa na wawekezaji wakigeni na wananchi kubakia kama watazamaji wanaolinda misitu lakini wasiojua faida kiasi gani inayopatikana baada ya kuuza oksjeni yao.

### SANAA/BURUDANI

Profesa Ruth anasema sanaa na michezo ya burudani ni sekta inayokua likini wasichana na mabinti wanaishia kutumiwa.

Wanashiriki lakini hawakui wanatumiwa wala hawafaidiki na kwamba kuna unyanyasaji zaidi kuliko mafanikio.

"Wanawake na dira tunataka dira itamke kuwa ifikapo 2050 vipaji vya wanawake wabunifu vikuzwe viwanufaishe na taifa na wasinyanyaswe. Tunataka vikuzwe kikamilifu na viwe na tija kwao ili wasiendelee kutumiwa na kudhalilishwa kwa sababu hawanufaiki." Anasema Prof. Ruth.

ELIMU

NA HALFANI CHUSI

# Teknolojia ya kisasa itakavyoipaisha chai

WAPENZI wa chai ya rangi wanafurahia ile nyeusi ambayo imezoeleka karibu kila mahali, lakini sasa Bodi ya Chai Tanzania (TBT), inapania kuleta chai ya kijani yenye ladha tofauti na bora kiafya.

TBT inaongeza vionjo kwenye chai kwa kuwekeza katika teknolojia ya kisasa ili pamoja na ladha na ubora inakusudia kuiwezesha chai ya Tanzania kutawala soko la kitaifa na kimataifa.

Ni hatua inayofanikishwa baada ya ziara ya kampuni mbili zinazowekeza kwenye chai kutoka Japan ziara inayowezesha pande mbili hizo kukubaliana kubadilishana ujuzi na namna ya kutumia teknolojia ya kisasa kuongeza chai.

Wajapani hao wanaonyesha teknolojia ya kutengeneza chai ya kijani na vifungashio bora zaidi jambo linaloikuna TBT inayoanza kuweka mipango ya kutumia teknolojia ya kisasa ikiamini italeta mapinduzi ya viwanda.

Katika video fupi Wajapani wanaonyesha namna wanavyotumia mitambo mbalimbali na mashine kulima na kuchakata chai, kuanzia shambani mpaka kiwandani kisha kumfikishia mlaji hatua ambayo ni somo kwa bodi.

Hii ni sawa na kusema, ziara iliyofanywa na TBT Japan nchini Japan Julai mwaka huu imeleta matokeo chanya kwa kufanikisha kushawishi kampuni za Kawasaki Kiko na Nasa Corporation, ambazo mbali na kubadilishana ujuzi zimefunza wakulima mengi kuhusu kilimo cha zao hilo.

Ni baada ya kutembelea baadhi ya mashamba yaliyoko Iringa na Njombe zikiwamwagia sifa wakulima na chai ya Tanzania kuwa inafaa pia kuzalishwa chai ya kijani badala ya nyeusi ambayo ndiyo majani yanayotumika nchini.

Ugeni huo, ukiwa mkoani Njombe unatembelea shamba la Kibena pamoja na kiwanda cha Lipton, mashamba ya Chama cha Ushirika cha Mkonge Mufindi na kuzungumza na wakulima.

Wageni kutoka Japan wakiongozana na baadhi ya viongozi kutoka Bodi ya Chai -Kaimu Mkurugenzi wa bodi, Beatrice Banzi pamoja na wataalamu wa Wizara ya Kilimo, kwa nyakati zote wageni hao, walionyesha kufurahishwa na namna zao hilo linavyolimwa kwa wingi nchini.

Katika Kituo cha Utafiti wa Chai Tanzania (TRIT) wanafurahia uwezo mkubwa wa utafiti wa kituo hicho ambapo kimefanya tafiti na kuzalisha majani ya chai yaliyowavutia kwa kuwa yanafaa katika uzalishaji wa chai ya kijani.

Wanasifu kuwa chai ya Tanzania ni bora na wameona yenye majani membamba ambayo ndio inahitajika zaidi Japan kwa ajili ya kutengeneza chai ya kijani.

Aidha, mitambo wanayoliyonayo inawezakuchakata majani membamba, hata mapana nayo ni ya kisasa nasifu ... akiwa ameshika jani la chai akitabasamu kwa bashasha.

Anawasihi wakulima waendelea kufanya uwekezaji katika chai ya majani membamba na kwamba ina soko kubwa Japan.

### WAPIMA CHAI

Wakati wanakagua chai katika maeneo hayo, waliipima kwa kutumia tepu kwa lengo la kulinganisha na mashine zao ili kuona kama ukubwa au udogo wake hautaathiri mashine zao wakati wa kuchakata.

Aidha walilenga kuona namna ya kutengeneza mashine za kuchakata chai hiyo zitakazoendana na uhalisisa wa chai inayozalishwa nchini.

Beatrice Banzi kutoka TBT anasema ziara hiyo imekuwa ya mafanikio kwa kuwa Wajapan wamejionea mafanikio makubwa katika sekta hiyo.

Beatrice ambaye anawapitisha wageni hao kwa hatua kwa hatua katika mashamba na viwanda, anasema kampuni hizo ni kubwa na ni wazi zitaleta matokeo chanya katika kukuza zao hilo.

Awali akiupokea ugeni huo katika ofisi za bodi hiyo jijini Dar es Salaam anasema matarajio yao baada ya ziara hiyo ni kufanya mapinduzi makubwa ya viwanda.

"Tumeona wanasema hawana nguvu kazi ndipo wakaanza kubuni jinsi ya kufanya kazi za shambani bila watu kwa kutumia mapinduzi ya viwanda.

"Na sisi tunachokitarajia, ni mapinduzi ya viwanda kwa sababu wao hawana nguvu kazi sisi tunayo, lakini mitaji ya kuwalipa inakuwa shida kwa hiyo ni vizuri kutumia viwanda vyenye teknolojia ya kisasa ambavyo vitasaidia kupunguza gharama katika uzalishaji wa chai kama wanavyofanya wao," anasema Beatrice.

Anaongeza mbali na mapinduzi ya viwanda pia ni kuongeza ubora wa chai inayozalishwa nchini ili kulitawala soko la ndani na nje pia.

Ofisa Kilimo Idara ya Maendeleo ya Mazao Wizara ya Kilimo, Bahati Majaliwa, anasema mpango wa serikali ni kujenga viwanda vidogo vidogo vitakavyo wasaidia wakulima kusindika chai ili waweze kupata faida zaidi kutokana na mauzo.

"Wajapan wameipenda sana chai yenye majani membamba, na inazalishwa kwa wingi, katika maeneo mengi ya uzalishaji hapa nchini zaidi ya asilimia 80 ya chai hiyo inazalishwa.

"Wakulima waendelee kutunza mashamba yao vizuri ili kupata tija kutokana na majani watakayozalisha," anasema Majaliwa.

Mkakati wa Wizara ya Kilimo kwa sasa ni wakulima kusindika chai yao na kwamba mpango uliopo ni kuwekeza katika viwanda vya wakulima wadogo.

Anasema ujenzi wa viwanda kwa wakulima wadogo utawainua kiuchumi na kuzalisha chai yenye tija itakayoleta ushindani katika soko la kitaifa na kimataifa.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Utafiti wa Chai Tanzania (TRIT), Dk. Daniel Mgori, anasema hatua ya ugeni huo kutembelea katika kituo chao umewapa somo na kujua aina ya chai inayohitajika Japan.

Hapa Dk. Mgori, anawahakikishia Wajapan Wizara ya Kilimo, na Bodi ya Chai kwamba taasisi hiyo itafanya jitihada za kuzalisha kwa wingi miche yenye majani membamba ili wakulima waweze kulikamata soko lao.

Anasifu kampuni zilizowatembelea zimeongozana na wataalamu wa kutengeneza mashine za kuchakata chai na wamewapa ushauri wa namna ya kulima zao hilo.

Mwenyekiti wa Mashamba ya Chama cha Ushirika cha Mkonge, Balodaniel Mgonzo aliuomba ugeni huo, na serikali, kuwajengea kiwanda ili waachane na adha ya kuuza majani mabichi jambo linalowasababishia hasara.

Kufanikisha hilo, Mgonzo anasema tayari wametenga kiwanja chenye ukubwa wa hekari 12 ili atakapopatikana mwekezaji awajengee kiwanda waweze kuuza majani makavu.

Anasema wanakabiliana na changamoto ya malipo kidogo, ukilinganishwa na gharama za uendeshaji wa mashamba.

"Tunawakaribisha Wajapan waliokuja kututembelea leo, wajenge viwanda wanavyotaka na kama eneo tulilotenga halitatosha kuna sehemu jirani ya wakulima wapo tayari kujitolea," anasema Mgonzo.

Meneja Masoko TBT, Selemani Chillo, anawatoa shaka wakulima kwamba hali ya masoko ya chai nchini inazidi kuimarika na tayari wameshafungua masoko katika nchi za Omani, Sudan, na sasa mkakati walionao ni kufungua mengine katika nchi za Kiarabu.

Selemani anasema walipokwenda Japan waliwashawishi kuja nchini kuangalia fursa mbalimbali za chai, na kujifunza kutoka kwao teknolojia wanayoitumia iweze kutumika nchini katika kuongeza thamani ya chai na soko.

### WAWEKEZAJI WAITWA

Wakati huo, Naibu Katibu Mkuu wa Wizara ya Kilimo anayesimamia Maendeleo ya Mazao, Dk. Hussein Omar, anawataka wawekezaji kujitokeza kuwekeza kwenye sekta ya chai kuiinua ili achangie pato la taifa.

Dk. Omar anasema iwapo wawekezaji watajitokeza kwa wingi zaidi kuwekeza kwenye mnyororo mzima wa chai hususan katika kufungua viwanda vya uchakataji na ufungashaji wakulima wengi wa chai watanufaika.

Anasema, sekta ya chai ina fursa lukuki na zote hizi zinaweza kuiinua hivyo ni imani ya wizara kuwa kampuni za Japan kwa kuwa ni za uchakataji na ufungaji zikinunua moja kwa moja chai za wakulima watakuwa na soko la uhakika na wigo mpana zaidi wa kuuza zao hilo.



Wawekezaji kutoka Japan na baadhi ya viongozi wa TBT wakiwa katika ziara ya mashamba ya chai. **PICHA: HALFANI CHUSI**

ELIMU

NA MWANDISHI WETU

# Raha ya barabara nzuri Dar inapogeuka karaha ya usafiri

DAR ES SALAAM imejaa barabara nzuri karibu kila upande pia kuna mtandao mkubwa wa njia za mabasi ya mwendo wa haraka. Hakika inapendeza kutiririka na 'motokaa' ndani ya barabara za lami lakini kwenye uzuri hapakosi kasoro.

Uzuri huo wa barabara unakuwa kero kwa watumiaji kutokana na kila saa kukoswa koswa na ajali za kila mara hasa za bodaboda, bajaji kadhalika msongamano uliokithiri hasa jioni kwenye vituo vya mabasi.

Mojawapo ni Mbezi Magufuli kunakomfanya msafiri au mtumia barabara akereke na foleni zinazomsonga karibu kila wakati asubuhi, mchana na pia nyakati za sikukuu na hata mwisho wa juma.

Lakini pia upo utitiri wa vyombo vya moto kwa vile kila upande kipo chombo kinachomghasi kulia na kushoto, nyuma na mbele anasongwa na pikipiki, guta, baiskeli, lori, magari madogo, daladala, mabasi yaendayokasi ya masafa na malori.

Unafika kipindi kituo hasa Mbezi Lousi au kwa Magufuli nyakati za asubuhi huwezi kuingia wala kutokea.

Hali hii inamfanya mtumiaji asione uzuri wa maelezo kuwa Dar es Salaam ina mtandao kabambe wa barabara na pia inamkera asipende usafiri wake ambao ni kama gereza ndani ya barabara.

Mwaka jana 2023 Rais Samia Suluhu Hassan akiwahutubia maofisa wa Jeshi la Polisi anaahidi kuweka kamera za usalama kwenye barabara kuu kudhibiti na kupunguza uhalifu na ajali.

Ukweli unabaki kuwa ajali nyingi zinapatikana Dar es Salaam kwenye mtandao wa barabara bora na nyingi. Takwimu za Jeshi la Polisi za mwaka 2023 zinathibitisha hilo.

Takwimu hizo za hali ya uhalifu na matukio ya usalama barabarani ya Januari hadi Desemba 2023 zilitokea ajali 1,733 zilizoua Watanzania 1,645 na kujeruhi 2689.

Kadhalika zinaonyesha kuwa mwaka 2022 kipindi kama hicho ziliripotiwa ajali 1,545 na kwamba lipo ongezeko. Kwenye bodaboda zilikuwa 431 na wakati 2023 zikiongezeka hadi 448.

Polisi wanasema kitaifa Ilala ni mkoa unaoongoza kiajali zikifikia 514,951, Kinondoni 259,707 na Temeke ajali 229,532 ziliripotiwa. Jeshi hilo linataja ubovu wa barabara na vyombo pamoja na makosa ya kibinadamu kuwa ni chombo.

Mwezi Septemba kila mwaka mambo ya usalama barabarani hupewa kipaumbele Jeshi la Polisi na wadau, wakikumbusha usalama wa maisha na mali za watumia barabara lengo ni kupunguza ajali, kuuelimisha umma juu ya matumizi salama ya barabara, vyombo madhubuti, kutumia leseni na kuwa na madereva wataaluma wanaoendesha kwa kujihami na kwa usalama.

Lakini mwaka huu unapoelekea ukingoni kero ya usafiri barabarani ya kuwa na makondakta, madereva na daladala chafu iko pale pale.

Ni kwa nadra kuwakuta madereva na makondakta wa daladala wakiwa nadhifu. Ni kero kwa abiria kukutana na kondakta mchafu kuanzia mavazi, viatu kinywa na hata mikono anayomkaribisha nayo mteja kwenye daladala ni michafu.

Mbona wiki ya usalama haisaidii kuhimiza usafi wa wahudumu wa kwenye daladala? Magari ni machafu kupindukia mengine yana viti vya vyuma na mbao sponji zimetoka, yanaendeshwa na dereva asiyechana nywele, asiyevaa kwa unadhifu aliyevalia nguo kadhaa zote zikiwa zimechakaa, ana fulana chafu ndani, suti imeraruka na wakati mwingine kiunoni amevaa mkanda wa kufungia raba, katani au kipande cha zipu.

Makamanda mnasimama barabarani kagueni sare sisitizeni kuweka mabasi katika hali ya usafi. Pia vioo na madirisha ya daladala nyingine ni vibovu na ikinyesha mvua maji yanavujia ndani abiria wanalowana kwa vile dari ni bovu.



Fujo zinazotokana na vurugu za msongmano barabarani. **PICHA: MTANDAO**

### VURUGU BARABARANI

Wakati mwingine barabara zinatumiwa kienyeji kwa mfano wanaobeba mkaa wanafunga magunia kadhaa kwenye pikipiki hawaoni nyuma tena wanajaa barabara nzima bila woga.

Makamanda lazima barabara ziwe na mpangilio wasaidieni watumiaji wajisikie salama. Jitihada za kuweka maeneo maalumu ya teksi, bajaji na pikipiki zimezifanya barabara kuwa na kitisho zaidi maana boda na bajaji zinaegeshwa kila mahali.

Wapo wanaojibanza kwenye kona kwa mfano makutano ya njia nne zinazokwenda Goba, Madale, Kimara na Matosa, kadhalika kila eneo linakuwa na pikipiki na bajaji ambazo huingia barabarani wakati mwingine kuzuia mabasi hasa daladala kuegeshwa.

Haipendezi kuona boda ziko kila mahala, zikiwakera watembea kwa miguu na wapanda magari. Mathalani abiria akifika Mbezi anakutana na makundi ya vijana wenye misuli na nguvu wakiwafukuza abiria ili kuwapa usafiri wa kwenda mikoani.

Kikosi cha Usalama Barabarani, hili limekaaje? Mbona watu hawa wanazidi kujikusanya Mbezi? Hili nalo halina tiba kama kuna ufumbuzi kwanini vijana kama hao wamejazana kituoni hata kukwamisha magari na abiria?

Boda na bajaji zimekuwa kero zinaingia barabarani bila mpangilio na kusababisha watu kugongwa kutokana na kuchanganyikiwa kushindwa kulipisha gari kubwa ama boda ambazo huranda barabara muda wote bila kujali kuwa hata magari mengine yapo. Mwaka mpya unavyokaribia kuna haja ya kufanya juhudi zaidi ili kuwa na maeneo maalumu ya boda boda na bajaji kuzizuia zisijirundike vituoni na kukwamisha watu kutumia maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya kusubiri na kupanda daladala.

Licha ya viongozi kuzungumzia mara kwa mara kuhusu malalamiko ya kuwapo trafiki barabarani na kuahidi kuwa wataweka kamera za kurekodi matukio bado walinzi wa usalama wanazidi kulalamikiwa kuwa wanafanya yanayowafaidisha zaidi na kuwaumiza wasafirishaji.

Kuna madai kuwa kinachotafutwa ni 'chochote' wasimamizi hao wanawatoa upepo madereva na kuna madai kuwa wanaelekezwa maeneo maalumu kuweka kitu kidogo vikiwamo vibanda vya mawakala simu. Mambo hayo yanawafanya kudharaulika kuwa lengo siku kuwa na usalama bali ni kuapata 'kitu kidogo'.

Ikumbukwe usalama wa barabara ukiegemea zaidi eneo hilo ni kama taifa linaambiwa liendelee kuvumilia ajali zaidi, majeruhi watazidi kuongezeka, walemavu na vifo zaidi vya barabarani pamoja na uharibifu wa miundombinu.

Ni kwa sababu magari mabovu yanajaa barabarani, madereva wasiojali wanaendesha, pikipiki zinavunja sheria alimradi kila mtu anafanya apendavyo.



## IFM kuanza kusaka wanafunzi sekondari

**Na Renatha Msungu**
DODOMA

CHUO cha Usimamizi wa Fedha nchini (IFM) kimetangaza mkakati wake wa kusambaza madaftari kwa shule 184 za sekondari nchini kushawishi wanafunzi kupenda masomo ya hisabati, sayansi na kujiunga nacho kuanzia mwaka ujao.

Mkakati huo umetengazwa na Mkuu wa IFM, Profesa Josephat Lotto katika hafla ya pamoja na wanafunzi waliosoma miaka ya nyuma katika chuo hicho kutoka maeneo mbalimbali nchini.

Profesa Lotto, alisema mkakati huo unalenga kushawishi wanafunzi wa shule hizo kupenda kusoma masomo hayo hususani hisabati ambalo kwa sehemu kubwa ndilo linalofundishwa chuoni hapo.

Alifafanua kuwa madaftari hayo yatawekwa nembo ya chuo hicho ili mwanafunzi anapopewa asome kwa bidii hisabati na kukumbuka kukichagua chuo hicho atakapohitimu masomo yake ya kiadato cha sita.

Alisema katika kutekeleza mkakati huo, alisema wanahitaji Sh. milioni 52.8 na kwamba kati hizo zimetolewa ahadi ya Sh. milioni 36 kutoka kwa wanafunzi waliosoma miaka ya nyuma katika chuo hicho.

Profesa Lotto aliwashukuru wanafunzi hao kwa ahadi hizo kwani utaisaidia kufanikisha kutekelezwa kwa mkakati huo na mingine ambayo haijabainishwa lengo la kuboresha chuo hiko kitaaluma.

Aliitaja mikoa sita ambayo wataanza kutekeleza mkakati huo kuwa ni Mwanza, Tabora, Kagera, Morogoro na Dodoma baada ya kupata ushirikiano kutoka kwa maofisa tawala.

# Vijiji vyagawiwa mitungi ya gesi

**Na Thobias Mwanakatwe,**
IKUNGI

MBUNGE wa Viti Maalum Mkoa wa Singida, Martha Gwau, amegawa mitungi ya gesi kwa wanawake mkoani hapa kwa ajili ya matumizi ya kupikia na kuondokana na nishati chafu.

Mbunge huyo ametoa msaada huo kwa wanawake hao wa vijiji vya kata za Ilongero, Kijota na Mtinko wilayani hapa na Kijiji cha Kideka Ikungi ikiwa ni sehemu ya kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan kuhamasisha matumizi ya nishati safi ya kupikia nchini.

Akizungumza juzi na wanawake hao, alisema ametoa mitungi hiyo ili waondokane na matumizi ya nishati chafu kwa ajili ya kupikia majumbani kama ambavyo Rais Samia anavyohimiza matumizi ya nishati safi ya kupikia.

"Rais Dk. Samia amelipa kipaumbele sana suala la matumizi ya nishati safi ya kupikia, anatamani kila mmoja aweze kutumia nishati hii ndio maana na sisi wasaidizi wake tunaendelea kumuunga mkono na leo nimekuja kutoa mitungi ya gesi," alisema mbunge huyo.

Aliwashukuru wananchi mkoani hapa kwa kujitokeza kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa hivi karibuni kwa amani na utulivu na kuwataka kuendelea kuilinda na kuidumisha kama njia ya kuwaenzi waasisi wa taifa la Tanzania.

Aliwashukuru viongozi akiwamo Mbunge wa Singida Kaskazini, Ramadhani Ighondo kwa kazi nzuri anayoendelea kufanya jimboni humo kwa kushirikana na madiwani.

Mbunge huyo pia alitoa mitungi ya gesi katika Kijiji cha Kideka kilichoko Kata ya Puma kwa wafanyabiashara na kofia za kujikinga na jua.

Alipongeza juhudi za serikali kuhakikisha ifikapo mwaka 2034, asilimia 80 ya Watanzania wawe wanatumia nishati safi ya kupikia, kutunza na kuhifadhi mazingira.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Ikungi, Mika Likapakapa, alisema mradi huo ni utekelezaji wa Ilani ya CCM kuimarisha sekta ya nishati kwa kuwa na nishati safi ya kupikia na kuhifadhi mazingira.



Wananchi wa kata za Ilongero, Kijota na Mtiko wilayani Singida wakiwa na mitungi ya gesi waliyokabidhiwa juzi na Mbunge wa Viti Maalum Mkoa wa Singida, Martha Gwau, ikiwa na lengo la kumuunga mkono Rais Samia Suluhu Hassan katika matumizi ya nishati safi ya kupikia. **PICHA: THOBIAS MWANAKATWE**

# TAKUKURU yatangaza vipaumbele

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), mkoani hapa imetaja vipaumbele saba vya utekelezaji majukumu yake ili kudhibiti ubadhirifu wa fedha zinazotolewa na serikali kwa utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mkuu wa TAKUKURU mkoani hapa, Victor Swella alivitaja vipaumbele hivyo taarifa yake ya utendaji kazi wa taasisi hiyo kwa kipindi kijacho.

Kwa mujibu wa Swella, vipaumbele hivyo ni kuongeza kasi ya uelimishana madhara ya rushwa katika makundi tofauti ili kuwawezesha wananchi kujua wajibu wao kuzuia.

Kuongeza kasi ya uelimishaji kwa kutumia njia mbalimbali hususani katika makundi ya vijana ambao ndio nguvu ya taifa na viongozi wa baadaye.

Kuongeza kasi ya kufanya chambuzi za mifumo maeneo yanayolalamikiwa zaidi kwenye utoaji huduma kwa wananchi.

Kuendelea kuelimisha jamii hususani kundi la vijana kupitia ushirikiano uliopo kati ya taasisi hiyo, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya mkoani hapa.

Kuongeza kasi ya kuwafikia wadau kupitia programu ya TAKUKURU rafiki ili kuibua kero zao na kuzipatia ufumbuzi.

# Madiwani Makete, Igunga wajifunza utekelezaji miradi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

MKUU wa Wilaya ya Makete, Juma Sweda mkoani Njombe, amewataka madiwani Halmashauri ya Makete na Igunga waliotembelea kujifunza utekelezaji wa miradi ya maendeleo jijini hapa kuitumia kama darasa katika maeneo yao ili walete tija.

Sweda alitoa rai hiyo juzi baada ya madiwani hao kutoka Makete na Igunga kukamilisha ziara yao ya mafunzo ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ndani ya Halmashauri ya Jiji la Dodoma.

Alisema madiwani hao wanapaswa kutumia ziara hiyo kujifunza na kuongeza ufanisi na mapato kwa kushirikiana na wananchi ili kukuza uchumi katika maeneo yao.

Alizitaka halmashauri hizo kubuni vyanzo vingine vya mapato kama ambavyo wamejifunza katika ziara hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Igunga, Swela Hamid, alisema ni imani yake madiwani wamepata ujuzi na watasaidia maeneo yao kufanya uwekezaji katika miundombinu kwenye maeneo yao.

Hamid, alisema walichojifunza kitasaidia halmashauri zao kujiendeshabila kutegemea fedha kutoka serikali kuu na kuinua uchumi.

Meya wa Jiji la Dodoma, Profesa Davis Mwamfupe, aliwataka madiwani wa halmashauri hizo kushirikiana katika kazi, kusimamia miradi na kufanikisha ukusanyaji wa mapato.

"Siri ya mafanikio ya halmashauri zetu ni ushirikiano na usimamizi na uaminifu wa kwenye miradi iliyopo, hapo ndipo mnapoweza kuongeza mapato na wananchi wakapatiwa maendeleo kiuchumi," alisema Mwamfupe.

Katika ziara hiyo madiwani hao walifuatana na wenyeviti wa halmashauri hizo, wakuu wa idara na vitengo mbalimbali.



# Waraka kupinga mauaji kusomwa kwenye makanisa na misikitini

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

SERIKALI mkoani hapa imeomba waraka kupinga kukithiri kwa mauaji wakati wa msimu wa sikukuu za Krismas na Mwaka Mpya kutokana na takwimu zake kuwa za juu kwa kipindi cha mwaka huu.

Waraka huo mbali na kupelekwa kwa viongozi wa dini, jukumu hilo pia wamepewa viongozi wa siasa, mila na jamii kushiriki kuelimisha wananchi ambao wako karibu nao kuondokana na imani za kushirikina, visasi, tamaa za mali na madaraka ambavyo ni chanzo cha mauaji hayo ambayo yametikisa mwaka huu.

Katika waraka huo maalumu wa Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka kuhusu udumavu, ukatili wa kijinsia na mauaji, ameomba usomwe kwenye nyumba zote za ibada kesho wakati wa ibada ya sikuuu ya Krismas na Januari Mosi, wiki ijayo wakati wa mwaka mpya wa 2025.

Mtaka pia ameomba waraka huo pia usomwe kwenye nyumba za ibada Ijumaa ya Januari 3 hadi 5 mwakani.

Katika waraka huo, alisema kwa masikitiko mwaka huu kumekuwa na ongezeko la matukio ya ukatili wa kijinsia na mauaji katika baadhi ya maeneo ya mkoa huo.

Alisema vitendo hivyo ni ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu na vinasababisha majeraha ya kimwili na kisaikolojia kwa waathirika.

"Vitendo hivi vinafedhehesha taswira nzuri ya mkoa wetu na vinastahili kulaaniwa kwa nguvu zote na wana Njombe wote kwani si utamaduni wa mila yetu, si utaifa na wala si Utanzania na ni vitendo visivyobeba sura halisi ya Mungu," alisema Mtaka.

Kwa upande mwingine, aliviagiza vyombo vya dola kuchukua hatua kali za kisheria dhidi ya watu wanaohusika na vitendo hivyo ili haki iweze kuonekana na kutomezwa kwenye jamii.

"Napenda kusisitiza vyombo vyetu vya utoaji haki vitakuwa na msaada mkubwa kwa waathirika wakaothibitika kushiriki matendo haya ya fedheha na yanayo tweza utu wa binadamu, jambo kubwa wananchi watoe ushirikiano wa taarifa kwenye ofisi za serikali," alisema Mtaka.

Kuhusu kupambana na udumavu, Mtaka, alisema mkoa huo una kiwango kikubwa kwa asilimia 50.4 kwa watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa mujibu wa Utafiti wa Afya, Demografia na Viashiria vya Malaria mwaka 2022.

"Ni hali inayosikitisha na inayohitaji juhudi za dhati kutoka kwetu sote kwa sababu udumavu unaathari kubwa katika ukuaji wa mwili na akili ya mtoto, unachangia maendeleo duni shuleni, uwezo mdogo wa kufikiri, kujifunza na ubunifu," alisema Mtaka.

Alibainisha kuwa serikali ya mkoa huo kwa kushirikiana na wadau, wako kwenye kampeni maalum ya kuongeza kasi ya kutokomeza udumavu wa lishe ya mwanao, mafaniko yake inayoongozwa na kauli mbiu kujaza tumbo si lishe, jali unachomlisha.



Sehemu ya kaya 125 zilizopo Msomera, Kata ya Misima, wilayani Handeni, zikipokea magunia ya mahindi yaliyotolewa na Mamlaka ya Hifadhi ya Ngorongoro (NCAA). Serikali kupitia NCAA, ilitoa msaada huo wa mahindi kwa Wamaasai waliohamia Msomera kutoka Ngorongoro kwa hiari ili kuwasaidia kwa muda wa miezi 18. Kila kaya inapata magunia mawili ya mahindi. **PICHA: CHEJI BAKARI**

# TASAF yapunguza vifo Peramiho

**Na Faustine Feliciane,** SONGEA

KUKAMILIKA kwa ujenzi wa nyumba za watumishi wa afya katika Kijiji cha Mdundwaro Kata ya Peramiho wilayani hapa Mkoa wa Ruvuma kumepunguza adha ya upatikanaji wa huduma za afya na vifo vya wananchi kwa kukosa matibabu.

Wakizungumza na waandishi wa habari kijijini hapo, wakazi wa maeneo hayo walisema uwepo wa watoa huduma katika kituo hicho kwa muda wote kumeboresha upatikanaji wa huduma za afya kwa muda wote.

"Awali huduma katika kituo hiki ilikuwa inatolewa kwa saa na kuna wakati watoa huduma wanakuwa hawapo hasa wakati wa mwishoni mwa wiki, wengi walikuwa wanakaa mbali, ilikuwa inatulazimu kusafiri kutoka kijijini kwenda Peramiho mjini au Songea, baadhi ya wagonjwa walikuwa wanapoteza maisha njiani."

"Kwa sasa watoa huduma wapo kwa muda wote, hivyo hawana haja ya kusafiri kwenda mbali kufuata matibabu," alisema Agustino Luhwoga, Mkazi wa Kijiji cha Mdundwaro na Msimamizi wa kituo hicho.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji hicho, Zawadi Mlapone, alisema mradi wa ujenzi wa nyumba hizo, kisima cha maji na matundu nane ya vyoo umeendeshwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na kuboresha huduma za afya.

"Kwa sasa tunaomba Serikali au TASAF watusaidia gari la wagonjwa kuwasafirisha wale wanaotakiwa kwenda hospitali kubwa, Peramiho au Songea kwa ajili ya matibabu zaidi," alisema Zawadi.

Hata hivyo, aliishukuru TASAF na serikali kwa kuwajengea mradi huo.

Mratibu wa TASAF Manispaa ya Songea, Ahosana Ngunge, alisema mradi huo ulianza mwaka jana baada ya kuombwa na wananchi na kukamilika Machi mwaka huu.

"Mradi huu umeghalimu shilingi milioni 179 kujenga nyumba mbili za wafanyakazi wa kituo, matundu nane ya vyoo, kuchimba kisima na ujenzi wa kichomea taka," alisema.

Kaimu Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea, Hassan Mtamba, aliishukuru TASAF kwa mradi huo na kuahidi kushirikiana na wananchi kutunza miundombinu na kutatua kero zilizobaki.

# Wenyeviti vijiji, vitongoji wabebeshwa majukumu

**Na Elizabeth John,** WANGING'OMBE

MKUU wa Wilaya ya Wanging'ombe mkoani Njombe, Zakaria Mwansasu amewaagiza wenyeviti wa vijiji na vitongoji kushirikiana na serikali kutatua migogoro ya ardhi kwa haki kwenye maeneo yao.

Mwansasu alitoa agizo hilo jana wakati akifungua mafunzo ya wenyeviti wa vijiji na vitongoji katika ukumbi wa halmashauri ya wilaya hiyo.

Alisema ni vema viongozi hao wakatumia mikutano ya vijiji kuzungumzia miradi ya maendeleo, namna bora ya kujimilikisha ardhi kwa kufuata utararibu ili kudhibiti migogoro baina ya wananchi katika maeneo yao.

"Katika maeneo yetu hata ofisi yangu ya wilaya siku ambayo nashinda ofisini napokea watu watatu au wanne wakilalamika nimenyang'anywa shamba na shangazi, nimeporwa sijui nani kauza shamba, ninaomba katika hili niwaagize mkasimamie haki kutatua migogoro ya ardhi," alisema.

Vilevile, Mwansasu aliwaagiza wenyeviti hao kupiga marufuku imani za kishirikina katika maeneo yao kwa kuwa chanzo cha mauaji ya watu wasiokuwa na hatia.

Aliwataka kuepuka kuwa chanzo cha migogoro badala yake kwenda kutumikia wananchi kwa kuheshimu dhamana waliyopewa.

Katibu Tawala wa Wilaya hiyo, Veronica Sanga, aliwataka wenyeviti hao kuwa wavumilivu na kushughulikia malalamiko ya wananchi kwa kufuata utaratibu.

"Mtafundishwa namna ya uendeshaji wa vikao, lakini mtaenda kufundishwa matumizi ya lugha, sisi kama viongozi lazima tuwe na lugha nzuri zenye staha haijalishi unakumbana na changamoto nyingi kiasi gani," alisema Veronica.

Mhadhiri wa Chuo cha Serikali za Mitaa, Dk. Muhsin Danga, alisema mafunzo hayo ya siku moja lengo lake ni kuwawezesha wenyeviti hao kutambua majukumu yao wakati wa kuwatumikia wananchi.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo akiwamo, Winfrida Nyika, alisema mafunzo hayo yatawasaidia kuwa viongozi bora na kuahidi kutenda haki kwa wananchi.



# Vijana Tanga waonesha ubunifu Kenya

**Na Mwandishi Wetu,**
TANGA

VIJANA wapatao 30 wa Halmashauri ya Jiji la Tanga wameshiriki katika maonesho ya Wiki ya Ubunifu mjini Mombasa nchini Kenya kwa ajili ya kuonesha vipaji vyao na kujiajiri katika sekta binafsi.

Hayo yalisemwa na Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Balozi Batilda Buriani wakati akizungumza kwenye Jukwaa la Vijana Tanga Mradi wa Mtandao wa Fursa za Vijana Duniani (GOYN).

Balozi Batilda, alisema vijana hao walishiriki katika maonyesho hayo yalifanyika nchini humo Oktoba mwaka huu.

"Vijana takriban 30 wakiongozwa na viongozi wa Halmashauri ya Jiji la Tanga, walishiriki Wiki ya Ubunifu iliofanyika mjini Mombasa nchini Kenya yaliyoandaliwa na Taasisi ya Swahili Pot," alisema na kuongeza kuwa:

" Taasisi leo hii na yenyewe imewaleta takriban vijana 40 kuja kujifunza na kushirikiana na vijana wenzao kuandaa shughuli hii."

Alisema vijana wengine sita walishiriki katika Forum ya Vijana ya Duniani iliyofanyika India Novemba, mwaka huu.

"Mwakilishi wa Halmashauri na Vijana wote hawa walipata fursa ya kujifunza, kuonyesha bidhaa zao na kujenga mahusiano yenye kuleta tija katika kutumia fursa za kuajiriwa na kujiajiri," alisema.

Awali alilipongeza jukwaa hilo kwa kushirikisha na Programu ya Tanga Yetu na Mtandao wa Fursa za Vijana Duniani (GOYN) kwa kujitosa kupambana na tatizo la ukosefu wa ajira kwa vijana katika jiji hilo.

Hata hivyo, aliutaka uongozi wa halmashauri hiyo na serikali mkoani humo kutoa ushirikiano kwa taasisi hizo na wawekezaji ambao wanaonesha nia ya kuwasaidia vijana kuondokana na wimbi la ukosefu wa ajira.

**Balozi Batilda, alisema vijana hao walishiriki katika maonyesho hayo yalifanyika nchini humo Oktoba mwaka huu.**

# Jamii lawamani kukithiri ukatili kijinsia visiwani

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

JAMII imelaumiwa kuwa chanzo cha kukithiri kwa matukio ya ukatili wa kijinsia kunatokana na kuyafumbia macho kwa kuwalinda watuhumiwa.

Lawama hizo zimetolewa na wadau wa kupinga vitendo vya udhalilishaji wakati wa uwasilishaji wa ripoti ya takwimu za ukatili na udhalilishaji wa kijinsia kwa wanawake na watoto visiwani hapa.

Walisema ukatili wa kijinsia si kwamba hauwezi kuepukika, lakini jamii imekosa sehemu ya kupaza sauti na kukaa kimya, hivyo kuendelea kuathiri hasa wanawake na watoto.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Wazee, Siti Abass Ali, miongoni mwa wadau hao, alisema jamii na wazazi wanahitaji kujenga ushirikiano katika malezi ili kupunguza vitendo vya udhalilishaji.

Siti, alisema kuna umuhimu kwa jamii kwa kila mmoja kutoa ushirikiano ili kumaliza tatizo hilo.

Aliishauri jamii kurudi kwenye misingi ya malezi ya pamoja ya watoto ili kujenga jamii bora ya maisha kwa maendeleo ya taifa.

Wakili wa Serikali, Huda Othman Khamis, alisema jamii inatakiwa kushirikiana na mahakama na taasisi nyingine katika utoaji wa ushahidi ili kutokomeza vitendo hivyo katika jamii.

"Turudi katika mafundisho ya upendo na hali ya umoja na ya kumwona mtoto wa mwenzako kama wako. Tuwekeze katika elimu hasa ya kujilinda na kufundisha uhalisia wa matukio hayo," alisema.

Akiwasilisha ripoti ya matukio ya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia, Mkuu wa Divesheni ya Jinsia na Ajira Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, Sabina Raphael Daima, alisema matukio 136 yaliripotiwa kwa mwezi uliopita wa Novemba 2024.

Sabina, alisema idadi kubwa ya waathirika, walikuwa watoto sawa na asilimia 86.0, wakifuatiwa na wanawake asilimia 9.6 na wanaume asilimia 4.4.

Alisema kati ya watoto hao 177, wasichana walikuwa 100 sawa na asilimia 73.5 na wavulana walikuwa 17 asilimia 12.5.

Sabina aliitaja wilaya iliyoongoza kwa matukio hayo kuwa ni ya Magharibi 'A' 39, ikifuatiwa na Magharibi 'B' matukio 32` na ya tatu ni Micheweni na Mkoani kwa kila moja kuwa na matukio mawili.

Hata hivyo, Sabina, alisema takwimu zinaonyesha kuwa idadi ya matukio kwa mwezi uliopita imepungua kutoka 147 yaliyoripotiwa Oktoba.

Kwa mujibu wa Sabina, mashauri 15 ya udhalilishaji yalifunguliwa katika mahakama kwa mwezi uliopita, Mkoa wa Mjini Magharibi ukiongoza kwa kuwa na tisa sawa na asilimia 60.

Ripoti hiyo ya udhalilishaji imewasilishwa chini ya Shirika la Umoja wa Mataifa (UN) la kushughulia a masuala ya wanawake ikiwa ni jitihada za kupambana na vitendo hivyo dhidi yao, wasichana na watoto.



Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo Tabia Maulid Mwita (kushoto) na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Fatma Hamad Rajab, wakicheza wakati hafla ya uwekaji wa jiwe la msingi viwanja vya Maisara, Wilaya ya Mjini ikiwa ni shamrashamra za Maadhimisho ya Miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar. **PICHA: RAHAM SULEIMAN**

# Wahimizwa kutunza miundombinu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WANANCHI visiwani hapa wametakiwa kutunza miundombinu kwa manufaa yao na vizazi vya sasa na vijavyo kwa ajili ya kuwaletea maendeleo.

Rai hiyo ilitolewa jana na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais Katiba Sheria, Utumishi na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, wakati akizindua barabara ya Kidimni hadi Ubago yenye urefu wa kilometa 4.3, ikiwa ni shamrashamra za Miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Haroun, alisema serikali inaendelea kutekeleza ujenzi wa barabara za ndani zenye urefu wa kilometa 275.9 za Unguja kwa miezi 40.

Alisema kwa Unguja barabara zinazojengwa zitakuwa na urefu wa kilomita 140.95 na Pemba kilomita 134.95.

Aliwataka madereva kutumia barabara hizo kwa uangalifu zaidi kwa kufuata sheria za barabarani ili kuepuka ajali zinazotokea mara kwa mara na kusababisha vifo vya watu, majeruhi na ulemavu.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi Mawasiliano na Uchukuzi, Makame Machano Haji akitoa taarifa ya kuhusu ujenzi wa barabara hiyo, alisema unaunganisha barabara za mikoa ya Kusini na Kaskazini Unguja.

Haji, alisema barabara hiyo ilianza kujengwa na makandarasi wa Kampuni ya IRIS na MAWI, Novemba mwaka huu.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohammed, alisema barabara hiyo ni miongoni mwa miradi 16 ya kimkakati ikiwa ni Utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya 2020/2025 kwa ajili ya kuleta maendeleo kwa wananchi na mabadiliko katika taifa.

Mbunge wa Uzini, Khamis Hamza Khamis, aliwataka wananchi kuthamini na kuitunza barabara hiyo kwa ajili ya kurahisisha shughuli za kijamii kwao na vizazi vijavyo.

"Adhma ya serikali ni kuboresha na kuleta maendeleo endelevu kwa taifa kupitia awamu ya nane ya Rais Dk Hussein Mwinyi, hivyo tuwe wazalendo wa kutunza mazingira yetu kuwa bora na miundombinu inayotuzunguza na hii ni kwa faida yetu wenyewe, " alisema Khamis ambaye ni Naibu Waziri wa Mazingira na Muungano.

# Gari la DC lapigwa mawe, nyumba za viongozi kijijini zavunjwa, watu 32 watiwa mbaroni

**Na Waandishi Wetu**

JESHI la Polisi Mkoa wa Rukwa linawashikilia watu 32 kwa tuhuma za kufanya vurugu, kujeruhi watu wawili na kuharibu mali katika mkutano wa hadhara wa Mkuu wa Wilaya ya Nkasi, Peter Lijualikali.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Polisi, SACP Shadrack Masija, ilisema kuwa kati ya watuhumiwa hao wanaume ni 25, wanawake ni wanane na wote wanatuhumiwa kufanya fujo, kuharibu mali na kupiga watu.

Kamanda Masija alisema matukio hayo yalitokea Desemba 19, mwaka huu, saa tisa alasiri katika Kijiji cha Taramila, Kata ya Mihula Wilaya ya Nkasi, baada ya Mkuu wa wilaya hiyo, kufanya mkutano wa hadhara kijijini hapo uliolenga kuhimiza shughuli za maendeleo na mshikamano.

"Katika mkutano ule wananchi walijitokeza wengi zaidi ya 500 na wakati mkutano unakaribia mwisho, walifanya vurugu kwa kurusha mawe na fataki na walivunja vioo vya gari la Mkuu wa wilaya ambayo ni mali ya serikali anayoitumia kwa shughuli za kikazi.

"Pia walivunja nyumba ya Mwenyekiti wa kijiji hicho, Fortunatus Subasio, walivunja vyombo na kupora fedha zaidi ya Shilingi milioni sita, walivunja nyumba ya serikali ya kijiji anayoishi mwalimu mkuu wa kijiji hicho, pamoja na samani za ndani ikiwamo televisheni yake," alisema.

Kamanda Mashija alitaja mali nyingine zilizoharibiwa ni pikipiki iliyokuwa inatumiwa na askari wa Jeshi la Polisi ambaye ni Mkaguzi wa Kata ya Mihula pamoja na kujeruhi watu wawili wote wakazi wa kijiji hicho.

Aidha, Kamanda Masija alitoa wito kwa wananchi ambao walihusika katika tukio hilo ambao wamekimbia, kujisalimisha kabla hawajakamatwa.

"Nitoe wito kwa wananchi wa kijiji hicho, kwamba wale ambao wamekimbia huku na huku wakiogopa mkono wa sheria, niwatake warudi kijijini waendelee tu na shughuli zao za maendeleo, lakini Jeshi la Polisi linaendelea kuwasaka wale hasa waliohusika na matukio hayo niliyoyasema," alisema na kuongeza:

"Nitoe wito kwa wale wanaojua kwamba walishiriki wajisalimishe katika Kituo cha Polisi Wilaya ya Nkasi na kituo cha Polisi Sumbawanga kwani matukio hayo yalifanyika kweupe, kwa hiyo tunawatambua, wasijifiche, tutawasaka ili mkono wa sheria uchukue mkono wake."

Wakati huohuo, Jeshi la Polisi mkoani Dodoma limefanya operesheni na kukamata vitu mbalimbali vinavyodaiwa kuwa vya wizi.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi mkoani hapa, George Katabazi, alitaja vitu hivyo kuwa ni silaha aina ya pisto ikiwa na risasi 14, pikipiki 31, bangi, mirungi na gari ndogo.

Alisema katika operesheni hiyo wamefanikiwa kumkamata mtuhumiwa James Charles (17), mkazi wa Makulu jijini hapa, anayesadikiwa kuwa ni panyaroad kutokana na kufanya uhalifu kwa kutumia vitu vyenye ncha kali.

"Tunawashukuru wananchi wa Dodoma kwa kuendelea kutoa ushirikiano kwa Jeshi la Polisi, hii inasaidia kubaini wahalifu walojificha kwa lengo la kufanya matukio ya uhalifu," alisema Katabazi.

Kuhusu mhalifu anayesadikiwa kuwa ni panyaroad, Kamanda Katabazi alisema Jeshi la Polisi linamshikilia mtuhumiwa huyo mwenye umri wa miaka (17) akiwa na vitu vyenye ncha kali ambavyo huvitumia kufanya uhalifu.

Alisema pamoja na kutumia taarifa za kiintelijensia wataendelea kutumia taarifa za wananchi katika kufanya msako ili kuhakikisha wakazi wa Dodoma wanakuwa salama wakati wote.




Wajumbe wa Mkutano Mkuu wa Jimbo la Magu wakisikiliza taarifa ya utekelezaji wa Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kwa kipindi cha mwaka 2020-2024 wilayani Magu, jana. **PICHA: OFISI YA NAIBU WAZIRI MKUU**

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

THE CATHOLIC DIOCESE OF IRINGA WANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA GARI YENYE USAJILI T 215 DLT ,KWA YEYOTE ATAEFANIKIWA KUIONA KADI HIYO ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHOPO KARIBU NAE POLISI TAARIFA PHQ/IRI/IRI/20364/2024.

**IN THE DISTRICT OF COURT OF BAGAMOYO**
**AT BAGAMOYO**
**PROBATE AND ADMINSTRATION CAUSE**
**NO 31608 OF 2024**
**In the matter of estate of the late**
**ALBERT ALBANO MUHANIKA**
**And**
**In the matter of application for Petition for letters of administration by**
**AFRED ALBANO MUHANIKA**

**GENERAL CITATION (Rule 75)**

All persons claiming to have interest in the estate of the late ALBERT ALBANO MUHANIKA are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of administration is made to the ALFRED ALBANO MUHANIKA, petitioner.

Objections to the grant should be filed on or before the 6th January, 2024.

Dated at Bagamoyo this 16th day of January, 2024

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE
BAGAMOYO

MARCAS DEBT COLLECTORS & AUCTIONEERS (T) LTD.

## NOTISI YA KULIPA DENI NA MNADA WA HADHARA

Kampuni ya **MARCAS DEBT COLLECTORS & AUCTIONEERS LTD**, kwa idhini tuliyopewa na **MTEJA WETU**, tunatoa notisi ya siku kumi na nne ya kulipa dhamana itauzwa kwa njia ya **MNADA WA HADHARA,** mnada utafanyika siku na tarehe kama inavyoonekana hapo chini. Mnada utafanyika kuanzia saa 6:00 mchana na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonyesha hapo chini.

| NA. | JINA LA MDAIWA | DHAMANA/MAHALI ILIPO | TAREHE YA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1. | JOSEPH PAUL LEYARO | HATI NAMBA: 2435 PLOT NO. 2, Kijiji cha Ikirevi, jijini Arusha. | Jumatatu, 6/01/2025 kuanzia saa 06:00 mchana |
| | | HATI NAMBA: 25806 PLOT NO. 621, Sombetini, Manispaa ya Arusha. | Jumatatu, 6/01/2025 kuanzia saa 06:00 mchana |
| | | HATI NAMBA: 23931 PLOT NO.790, Themi, Manispaa ya Arusha. | Jumatatu, 6/01/2025 kuanzia saa 06:00 mchana |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa "kama ilivyo".
2. Mnunuzi atatakiwa kulipia 25% ya bei ya mnada siku ya mnada na kiasi cha pesa kilichobaki kilipwe ndani ya siku 14, kinyume cha hapo kiasi kilichotolewa awali hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena
3. Gharama za kubadilisha hati miliki (transfer of ownership) na gharama nyingine ni za mnunuzi.
4. Ukaguzi wa dhamana utafanyika kuanzia siku ya tangazo hili kutoka kuanzia saa 02:00 asubuhi na kuendelea.
5. Kwa mawasiliano zaidi, piga simu na: **0752722222**

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MOSHI SUB – REGISTRY**
**AT MOSHI**
**MISCELLANEOUS LAND APPLICATION NO.25746 OF 2024**
**ADINANI MUSA MVUNGI........................1ST APPLICANT**
**ELISAMSONI SHABANI MSUYA ............. 2ND APPLICANT**
**ELIEZA ANGOVI MSUYA .........................3RD APPLICANT**
**EVALISTA DAVID MFINANGA..................4TH APPLICANT**
**VERSUS**
**MANGIO SECONDARY SCHOOL ..................1ST RESPONDENT**
**THE REGISTERED TRUSTEES OF**
**CHAMA CHA MAPINDUZI (CCM)...................2ND RESPONDENT**
**MWANGA DISTRICT COUNCIL.......................3RD RESPONDENT**
**ALHAJI YUSUPH MFINANGA.........................4TH RESPONDENT**
**HON.ATTORNEY GENERAL ..........................5TH RESPONDENT**

**TO: ALHAJI YUSUPH MFINANGA**
**NOTICE FOR MENTION**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention in the High Court of Tanzania at Moshi on 12th March, 2025 at 9:00 a.m before Honourable **L. M. MONGELLA,** Judge.

**WHEREAS:** Service on you has been ordered to be published in the Nipashe.
You may appear in person or by Advocate or agent dully authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely upon in support of your case.

**TAKE FURTHER NOTE THAT**: In default of your appearance on that day and time the court may proceed in your absence.

**GIVEN UNDER** my hand and seal of the Court this 11th day of December, 2024

DEPUTY REGISTRAR

## KUPOTEA KWA CHETI



**AMINA S SHABANI,** anatangaza kupotea kwa Cheti cha Kidato cha Sita chenye Index namba **S0949/0561** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia Shule ya Sekondari IRKISONGO .. Yeyote atakayekiona atoe taarifa Kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi **PHQ/ARU/ARU/47198/2024**

## KUPOTEA KWA CHETI



**VICTORIA CHARLES SANGWA,** Anatangaza kupotelewa na Cheti cha Kidato cha Nne Chenye Index Namba S0694/0025, Kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia shule ya sekondari Kanga Mwaka 2016.Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha Polisi.
**TAARIFA YA POLISI: PHQ/DOD/DOD/54756/2024**

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**SAID HAMDUNI JOSEPH** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 916 DPV** aina ya **NISSAN X-TRAIL.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu
Taarifa ya polisi .
**PHQ/SHI/KAH/12480/2024**

## KUPOTEA KWA KADI ZA PIKIPIKI

Ndugu **MDACHI KIMANYA CHOYO** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki MC 796 AJG yenye chassis Namba RB4055A00005 kwa yeyote atakayeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu nawe.
Taarifa Polisi:
**PHQ/TAN/TAN/13344/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI ZA GARI

**LUCAS MWESSY KAIGARULA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari namba za usajili T 209 CAD aina ya Toyota LANDCRUSEIR ,. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.
Taarifa ya Polisi:
**PHQ/DAR/ILA/283496/2024**

# Upinzani watishia kuitisha maandamano Msumbiji

**MAPUTO, Msumbiji**

WASIWASI umetanda nchini Msumbiji baada ya kiongozi wa upinzani, Venancio Mondlane, kudhamiria kuamsha vurugu nchini humo kwa kuitisha maandamano, ikiwa baraza la katiba litamthibitisha mgombea wa chama tawala, Daniel Chapo kuwa mshindi.

Ilielezwa jana kuwa macho ya Wasumbiji yameelekezwa kwa Baraza la Katiba ambako majaji wanatarajiwa kutoa maamuzi waliyofikia kuhusu hatima ya matokeo ya uchaguzi wa rais uliofanyika Oktoba 9, mwaka huu yaliyompa ushindi mgombea wa chama tawala Chapo.

Kiongozi wa upinzani Mondlane alidai kwamba uchaguzi huo ulikumbwa na udanganyifu na matokeo yaliyotangazwa na tume, yalichakachuliwa kumpendelea mgombea huyo wa chama tawala.

Alisema matokeo ya kura zilizohesababiwa na upande wake zinaonesha alishinda kura za kutosha kumpa ushindi wa kutwaa madaraka, na hivyo ndivyo anavyodhamiria kufanya.

Mondlane ambaye hayuko nchini Msumbiji, lakini anawaongoza wafuasi wake akiwa nje ya nchi, ametoa vitisho kwamba nchi hiyo itatumbukia kwenye vurugu ikiwa Baraza la Katiba haitotangaza kile anachosema ni matokeo halali.

Kupitia ujumbe wake kwenye mitandao ya kijamii, aliwaambia wafuasi wake "Baadhi ya watu walifikiri hatua ya upinzani ya kuyapinga matokeo ni porojo, au masikhara, sasa watapata mshangao Januari 15 watakaponiona Venancio Mondlane ninachukuwa madaraka."

Mwanasiasa huyo alisema maamuzi yatakayotolewa na baraza la katiba yataamua, ama kuipeleka Msumbiji kwenye hatima ya utulivu na amani au kuitumbukiza kwenye vurugu. Huku akiapa kuanzisha kile alichokiita harakati za vuguvugu jipya la mapambano ambalo halijawahi kuonekana nchini humo.

Nchi hiyo ya Kusini mwa Afrika imekuwa kwenye hali ya machafuko tangu tume ya uchaguzi ilipotangaza matokeo mnamo mwezi Oktoba yaliyompa ushindi mgombea wa Frelimo, chama kinachoshikilia madarakani tangu Msumbiji ilipopata uhuru kutoka kwa Wareno, mwaka 1975.

Rais wa sasa Fillipe Nyusi anakamilisha muda wake madarakani Januari 15 ambako anatarajiwa kuyakabidhi madaraka kwa kiongozi mpya aliyechaguliwa.

Hivi sasa Mondlane mwenye umri wa miaka 50 na anayevutia vijana wengi wa Msumbiji alikimbilia uhamishoni tangu alipouawa wakili wake Oktoba 19, katika tukio analodai lilifanywa na vikosi vya usalama vya taifa hilo, na bado haijafahamika ikiwa anadhamiria kurejea.

Mvutano huo wa matokeo ya uchaguzi nchini humo umesababisha kushuhudiwa maandamano makubwa yaliyotatiza shughuli katika miji ya taifa hilo, kuhujumu shughuli za viwanda na mitambo ya umeme huku pia yakizuia shughuli za kwenye mpaka kati ya Msumbiji na Afrika Kusini, na kupelekea nchi hiyo jirani kupata hasara kubwa katika shughuli za usafirishaji. Aidha, ilielezwa kuwa kutokana na maandamano yaliyoitishwa jana na Mondlane na hali ilivyo, serikali ya Marekani iliongeza tahadhari kwa raia wake dhidi ya kuelekea Msumbiji.

Vile vile, Kiongozi Mkuu wa Kanisa Katoliki Duniani Papa Francis, alitoa mwito wa kufanyika mazungumzo ya maridhiano na nia njema kuondoa hali ya kutoaminiana nchini Msumbiji.

Mchambuzi mmoja wa kisiasa aliyeko Maputo Johann Smith alisema kinachoshuhudiwa Msumbiji ni sawa na hali iliyoshuhudiwa katika mataifa ya Kaskazini mwa Afrika mwaka 2010, akiyaita matukio ya Msumbiji ni vuguvugu la mapambano Kusini mwa Afrika.

***DW***



Maofisa wa usalama nchini Msumbiji wakiwa barabarani kufanya doria ya kuzuia maandamano jana. **PICHA: MTANDAO**

## China yaionya Marekani kutoa misaada Taiwan

**BEIJING, China**

SERIKALI ya China imelionya taifa la Marekani kwamba linacheza na moto baada ya kutoa tangazo la kutaka kutoa misaada ya kijeshi pamoja na kuiuzia silaha Taiwan.

Ilielezwa kuwa juzi Rais wa Marekani, Joe Biden alitangaza utoaji wa hadi dola milioni 571 kupitia Wizara ya Ulinzi, kwa ajili ya vifaa na huduma za kijeshi pamoja na mafunzo ya kijeshi kwenye kisiwa cha Taiwan kinachojitawala, na ambacho Beijing inadai ni himaya yake.

Kwenye taarifa tofauti, Wizara ya Ulinzi ya Marekani ilisema mwishoni mwa wiki kwamba uuzaji wa silaha za kijeshi wa dola milioni 295 kwa Taiwan tayari umeidhinishwa.

Pia taarifa ya Wizara ya Mambo ya Nje ya China iliisisitiza Marekani kusitisha kutoa silaha kwa Taiwan pamoja na kusitisha kile imekitaja kuwa hatua hatari zinazohujumu amani na uthabiti kwenye mlango wa bahari wa Taiwan.

Ilielezwa kuwa msaada wa kijeshi pamoja na silaha kutoka Marekani zinalenga kuisaidia Taiwan kujilinda dhidi ya mashambulizi ya China.

Tangazo la msaada wa kijeshi wa dola milioni 571 kwa Taiwan umefuatia hatua ya Biden ya kuidhinisha msaada mwingine wa dola milioni 567 mwishoni mwa Septemba. Na kwamba msaada huo utatumika kununua takriban mifumo 300 ya mawasiliano ya kijeshi miongoni mwa vifaa vingine.

***VOA***

## Vifo vyafikia 94 Msumbiji

**MAYOTTE, Msumbiji**

VIFO vinavyotokana na maafa ya kimbunga Chido kilichopiga eneo la Mayotte nchini Msumbiji karibu na Bahari ya Hindi wiki iliyopita vimefikia 94 kutoka 76 vya awali.

Hiyo ni kwa mujibu wa shirika la kudhibiti majanga Msumbiji, na kwamba kimbunga hicho, ambacho kiliharibu eneo la kisiwa cha Ufaransa cha Mayotte kabla ya kupiga Bara la Afrika, pia kiliharibu nyumba 110,000.

Baada ya kutua kimbunga hicho kiliharibu mkoa wa kaskazini wa Cabo Delgado kwa mafuriko ya takriban kilomita 260 kwa saa, na kunyesha mvua ya milimita 250 kwa siku.

Ilielezwa kuwa sehemu hiyo ya kaskazini mwa Msumbiji inaharibiwa mara kwa mara na dhoruba za kitropiki na kupambana na machafuko kutoka kwa waasi wa Kiislam wa muda mrefu.

Mgombea urais wa chama tawala cha Frelimo Daniel Chapo, ambaye ushindi wake kwenye sanduku la kura mwezi Oktoba umelaaniwa na upinzani kama ulaghai alitembelea maeneo yaliyoathirika.

Siku saba baada ya kimbunga hicho kupiga Mayotte, watu 35 waliripotiwa kufa na wengine 2,500 kujeruhiwa kwenye visiwa hivyo, kulingana na Wizara ya Mambo ya Ndani ya Ufaransa.

Lakini inahofiwa idadi ya vifo huenda ikaongezeka kwa kiasi kikubwa kutokana na idadi kubwa ya wahamiaji wasio na vibali kutoka visiwa vya Comoro vilivyo karibu, ambao wana tabia ya kuishi katika vitongoji vingi vya mabanda vya Mayotte vilivyokumbwa na dhoruba.

Baada ya kukumba Msumbiji, kimbunga hicho kilihamia Malawi na kwamba kiliua watu 13 na kujeruhi karibu 30, kulingana na wakala wa kudhibiti majanga ya Malawi.

***TRT***

**Mgombea urais wa chama tawala cha Frelimo Daniel Chapo, ambaye ushindi wake kwenye sanduku la kura mwezi Oktoba umelaaniwa na upinzani kama ulaghai alitembelea maeneo yaliyoathirika.**

# Mashujaa FC kusajili mastraika, mabeki

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Klabu ya Mashujaa umesema wanatarajia kuongeza wachezaji wanne kwa ajili ya kukiongezea nguvu kikosi chao wakati wa usajili wa dirisha dogo, imethibitishwa.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Mashujaa, Athumani Amiri, alisema safu ambazo watazifanyia maboresho ni safu ya ushambuliaji na ulinzi.

Amiri alisema anaamini wakisajili nyota wapya wataifanya timu yao kurejea katika ushindani na hatimaye kufikia malengo waliyojiwekea msimu huu.

"Dirisha dogo tunatarajia kuongeza wachezaji wanne ambao tunaamini wataleta ushindani mkubwa ndani ya timu yetu, nawakumbusha bado malengo yetu yakiwa ni kushiriki mashindano ya kimataifa msimu ujao," alisema Amiri.

Meneja huyo aliongeza wanaendelea kufanya mazungumzo na wachezaji wanaowahitaji na kuweka wazi hawatasajili kwa kuangalia ‚ukubwa wa jina' isipokuwa wanaangalia viwango vya mchezaji husika kwa sasa.

Bosi huyo aliongeza kwa sasa kikosi chao kinaendelea na maandalizi kwa ajili ya kuelekea mchezo wao ujao unaofuata wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Dodoma Jiji FC ambao utachezwa Desemba 28, mwaka huu.

„Maandalizi yameshaanza, vijana wanaendelea vyema kwa sababu hata wale wachezaji wao waliokuwa majeruhi kwa sasa afya zao zimeimarika na wameanza kujifua na wenzao," Amiri alisema.

Aliongeza wanatarajia kuanza safari ya kuelekea Dodoma leo kwa ajili ya kuwapa muda wachezaji kuzoea hali ya hewa ili wasipate tabu wakati wa mchezo.

„Jumatano tunatarajia kuelekea Dodoma na tumelazimika kwenda mapema ili wachezaji wakazoee hali ya hewa kwa sababu Kigoma kuna baridi tofauti na Dar es Salaam, „ alisema.

Aliweka wazi wanatarajia mchezo huo utakuwa mgumu na wenye upinzani kutokana na maandalizi yaliyofanywa na timu zote mbili.

Simba yenye pointi 34 ndio vinara wa ligi hiyo huku KenGold inaburuza mkia ikiwa na pointi sita mkononi.

# MBEYA CITY YAWATIBULIA GEITA, YAIBEBA MTIBWA

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Mbeya City imerahisisha safari ya Mtibwa Sugar ya kutaka kurejea katika Ligi Kuu Tanzania Bara, baada ya kuifunga Geita Gold bao 1-0 katika mchezo wa Ligi ya Championship uliyochezwa kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya juzi.

Bao pekee katika mchezo huo lilifungwa na Kilaza Mazoea, dakika ya 62 na kuifanya timu hiyo kusogea juu hadi nafasi ya nne ya kwenye msimamo wa ligi hiyo, ikifikisha pointi 25.

Geita Gold ambayo ilishuka daraja msimu uliopita kama Mtibwa Sugar, imeonekana ndiyo timu pinzani zinazokabana koo juu ya msimamo, lakini kipigo cha bao 1-0 katika raundi ya 13 ya ligi hiyo, kimeifanya kubakia na pointi 27.

Wakati Geita Gold, ikisalia katika nafasi ya pili, Mtibwa Sugar bado imeendelea kukaa kileleni kwa tofauti na pointi tano chini ya anayemfuatia baada ya kupata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Bigman FC, mchezo uliochezwa kwenye Uwanja wa Manungu Complex, Morogoro.

Bao la pekee katika mchezo huo lilifungwa na Juma Luizio dakika ya 52 na kuzidi kujiwekea matumaini ya kurejea Ligi Kuu msimu ujao moja kwa moja bila kusubiria mechi za ‚play off'.

Ikumbukwe timu mbili zitakazomaliza ligi hiyo zikiwa juu, zitapanda Ligi Kuu Tanzania Bara moja kwa moja, huku ya tatu, na ya nne zikicheza mechi za mchujo, kabla ya kwenda kucheza ‚play off' zingine dhidi ya timu za Ligi Kuu.

Kipigo ilichokipata, Bigman, kinaifanya kubaki na pointi 18, ikisalia nafasi ya tisa ya msimamo wa ligi hiyo.

Biashara United nayo iliamka usingizini baada ya kutoa kipigo cha mabao 4-1 dhidi ya Green Warriors mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Karume, Musoma mkoani Mara.

Shukrani kwa mabao mawili ya Elias Maguri, Januari Benson na Daud Mbweni yaliyoipa ushindi na pointi tatu na kufikisha pointi 16, ikiwa nafasi ya 10 ya msimamo wa Ligi Kuu.

Polisi Tanzania pia ilipata ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Songea United kwenye Uwanja wa Ushirika, Moshi, na kujiwezesha kufikia pointi 16, ikiwa katika nafasi ya 11 kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16 kutoka mikoa mbalimbali.



Mshambuliaji wa Simba Queens, Jentrix Shikangwa (kulia), akijiandaa kumtoka beki wa Mashujaa Queens, Tabea Munga, katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania (TWPL), iliyochezwa kwenye Uwanja wa Kituo cha TFF Kigamboni, Dar es Salaam. Simba Queens ilipata ushindi wa mabao 2-0 na sasa ndio vinara wa ligi hiyo. **PICHA: SIMBA SC**

# Tenisi wenye ulemavu yaanza kujinoa

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa Timu ya Taifa ya mchezo wa tenisi kwa wenye ulemavu tayari imeanza maandalizi kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya kuwania tiketi ya kufuzu fainali ya Kombe la Dunia zitakazofanyika baadaye mwakani.

Mashindano kwa ajili ya nchi za Afrika kupata wawakilishi wa michuano hiyo ya dunia yatafanyika kuanzia Februari 2 na 25, mwakani nchini Morocco.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Riziki Salum, alisema mashindano yatashirikisha timu kutoka mataifa mbalimbali kwa timu za wanaume na wanawake.

"Maandalizi kuelekea katika mashindano hayo yameanza, tunatarajia ifikapo Januari mwakani tutakuwa na mashindano ambayo yatatusaidia kupata wachezaji wenye viwango ambao watаunda timu imara itakayokwenda kuiwakilisha nchi yetu," alisema Salum.

Aliongeza timu hiyo ina wachezaji wenye viwango vya juu isipokuwa wanashindwa kuvitumia kutokana na kukosa kuwezeshwa.

Kocha huyo ameziomba taasisi na makampuni mbalimbali kujitokeza kuwasaidia ili kufanikisha wanaenda katika michuano hiyo huko Morocco.

"Tunawaomba wadau wa michezo kutoka sehemu mbalimbali watuunge mkono ili tuweze kwenda kuipeperusha vyema bendera ya Tanzania kwa kushika nafasi ya za juu," alisema Salumu.

## ZISIKUPITE

### PEDRO HAUZWI JANUARI

MPANGO wa Liverpool wa kumnunua mshambuliaji wa Brighton na Brazil, Joao Pedro, huenda ukalazimika kusubiri hadi msimu wa joto kwa sababu matakwa ya Seagulls hao kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 yatafanya uhamisho wa Januari kuwa mgumu. ***(Football Insider)***

### ISAK ATAKIWA PSG

KLABU ya Paris St-Germain ipo tayari kulipa euro milioni 100 ili kumsajili mshambuliaji wa Newcastle United ambaye ni raia wa Sweden, Alexander Isak mwenye umri wa miaka 25. ***(Fichajes.net)***

### WILLIAMS AGEUKA LULU

PSG pia inatazamia kulipa euro milioni 58 kama kifungu cha kutolewa kwa Athletic Bilbao kwa winga wa Hispania, Nico Williams - lakini Manchester United na Barcelona pia wanamtaka mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22. ***(El Desmarque)***

### DE JONG NJIA MOJA

BARCELONA imepoteza imani kwa kiungo wa kati wa Uholanzi, Frenkie de Jong, na inaonekana kuna uwezekano mkubwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 akaondoka katika klabu hiyo ya Hispania. (Relevo)

### GOMEZ ANUKIA LEICESTER

KLABU ya Leicester City inapanga mpango wa kutoa pauni milioni nane ili kumnunua kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Argentina, Valentin Gomez, mwenye umri wa miaka 21, kutoka Velez Sarsfield. ***(Sun)***

### GARCIA ANOGEWA BARCA

NEWCASTLE United ni moja ya klabu zinazomtaka beki wa Barcelona, Eric Garcia, mwenye umri wa miaka 23, lakini mchezaji huyo wa zamani wa Manchester City anataka kubakia Nou Camp kupigania nafasi katika kikosi cha kwanza. ***(Sport)***

### BESTE AKARIBIA PALACE

KLABU ya Crystal Palace inataka kumsajili kiungo wa kati wa Benfica, Jan-Niklas Beste mwenye umri wa miaka 25 ambaye ni raia wa Ujerumani, katika dirisha la Januari. ***(Sky Sports)***

### MARIN KUTUA MADRID

REAL Madrid inamfikiria beki wa kati wa Hispania, Rafa Marin, mwenye umri wa miaka 22, ambaye alifanya mazoezi katika akademi yao ya vijana na kwa sasa anachezea Napoli. ***(Fichajes.net)***

### MCBURNIE KUTUA ROVERS

KLABU za Blackburn Rovers na Burnley zinataka kumsajili mshambuliaji wa zamani wa Sheffield United mzaliwa wa Scotland, Oli McBurnie, mwenye umri wa miaka 28, kutoka Las Palmas ya Hispania. ***(Sun)***

### YAMAL KUJIFUNGA BARCA

WINGA wa Timu ya Taifa ya Hispania, Lamine Yamal mwenye umri wa miaka 17 anakaribia kuongeza mkataba wake na Barcelona hadi kufikia mwaka 2030. ***(Nicolo Schira)***

### WILSON KUONDOKA

KLABU ya Newcastle itamruhusu mshambuliaji wa England, Callum Wilson mwenye umri wa miaka 32, kuondoka huru mkataba wake utakapokamilika mwishoni mwa msimu huu. ***(Football Insider)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MBAPPE: NITAFANYA MAZURI ZAIDI MADRID

Mshambuliaji huyo asema kwa sasa ameshazoeana vyema na...

**MADRIS, Hispania**

KYLIAN Mbappé amesema alijisikia vibaya kwa kukosa penalti muhimu kwa Real Madrid mapema mwezi huu, akisema „naweza kufanya mengi zaidi" baada ya juzi kufunga katika ushindi wa mabao 4-2 wa timu hiyo wa LaLiga dhidi ya Sevilla.

Mshambuliaji huyo alifungua ukurasa wa mabao dhidi ya Sevilla kwenye Uwanja wa Bernabéu kwa bao lake la 14 msimu huu katika mashindano yote, na bao lake la sita kwenye ligi.

Hata hivyo, amekabiliwa na ukosoaji kwa uchezaji wake ikiwa ni pamoja na kufungwa kwa Madrid 2-1 na San Mamés mnamo Desemba 4, mwaka huu wakati Mbappé alishindwa kufunga.

"Naweza kufanya mengi zaidi," alisema Mbappé akiiambia Real Madrid TV.

"Ninajua nina mengi zaidi miguuni mwangu. Katika mechi chache zilizopita nimecheza vizuri zaidi. Mchezo wa Bilbao ulikuwa mzuri kwangu. Niligonga mwamba; nilikosa penalti. Ilikuwa wakati wa kutambua ni lazima nijitoe kwa kila kitu kwa ajili ya jezi hii."

Kosa la Mbappé dhidi ya Athletic lilikuja wiki moja baada ya kukosa penalti nyingine ikiokolewa na dhidi ya Liverpool kwenye Ligi ya Mabingwa, na siku chache baada ya kukataa nafasi ya kupiga penalti dhidi ya Getafe.

Mbappé tayari ameshinda mataji mawili akiwa na jezi ya Madrid -- akiinua UEFA Super Cup Agosti na Kombe la Klabu Bingwa ya Dunia ya FIFA wiki hii, akifunga katika ushindi wa 3-0 dhidi ya Pachuca ya Mexico nchini Qatar.

"Nadhani tumefahamiana zaidi," alisema Mbappé alipoulizwa juu ya kuongezeka kwake kwa kiwango.

"Nilikuja kwenye timu na hilo lilibadilisha mambo mengi, lakini sasa, kama kocha Carlo Ancelotti amesema, marekebisho yangu yamekamilika na ninajisikia vizuri. Tunaweza kuona uwanjani ninawaelewa wachezaji wenzangu vizuri zaidi, na timu nzima inacheza vizuri zaidi."

Madrid sasa wanaenda kwenye mapumziko ya Krismasi ya LaLiga wakiwa pointi moja tu nyuma ya viongozi Atletico na pointi mbili mbele ya wapinzani wao Barcelona.

## HABARI MICHEZO




# SALAH AWEKA REKODI YAKE YA KIBABE EPL

**LIVERPOOL, England**

IKIWA huu utakuwa msimu wa mwisho wa Mohamed Salah ndani ya Liverpool, basi ataondoka kwa kishindo kikubwa.

Fowadi huyo wa Misri alifunga mabao mawili na kutengeneza mengine mawili katika ushindi wa mabao 6-3 ambao Liverpool waliupata dhidi ya Tottenham Hotspur juzi na kuweka rekodi ya kufikisha mabao 15 na asisti 13 kabla ya Krismasi katika msimu wa Ligi Kuu England.

Mabao 15 yanamfanya kuongoza orodha ya wafungaji, huku nafasi ya pili ikishindwa na Erling Haaland wa Manchester City mwenye mabao 13.

Salah ameshinda Kiatu cha Dhahabu cha mfungaji bora wa Ligi Kuu mara tatu, msimu wa 2017-18 na 2018-19 na 2021-22.

"Sikuwaza kuhusu hilo kabla ya mchezo," alisema Salah baada ya mchezo huo.

„Lakini ni jambo linalonifurahisha na kujivunia. Ninaendelea kufanya kazi kwa bidii."

Huku mkataba wake ukitarajiwa kumalizika mwishoni mwa msimu huu, Salah aliulizwa baada ya mechi kama kulikuwa na habari kuhusu kuongeza mkataba na akajibu: „Hapana."

Kocha Mkuu wa Liverpool, Arne Slot, alisifu uchezaji wa timu yake, lakini alikiri alijisikia faraja kwa bao lao la sita na kujihakikishia pointi tatu.

"Mpaka dakika 60 hadi 65 kwa kweli nilifurahia kile nilichokiona," alisema Slot akiwaambia waandishi wa habari.

"Lakini pia uliona haijalishi wachezaji wana ubora kiasi gani, wanadhani sio lazima kukimbia tena."

# Amorim mambo magumu United

**MANCHESTER, England**

RUBEN Amorim amesema Manchester United iko katika „wakati mgumu" baada ya kufungwa mabao 3-0 na Bournemouth mechi iliyocheza kwenye Uwanja wa Old Trafford juzi.

Ni vipigo viwili mfululizo vya Ligi Kuu wakiwa Old Trafford baada ya Nottingham Forest kushinda mabao 3-2 mapema mwezi huu.

„Ni wakati mgumu lakini lazima tukabiliane nayo na kujiandaa kwa mchezo ujao," alisema Amorim akiwaambia waandishi wa habari.

„Ni jukumu langu kuwafundisha. Bila shaka tunataka kuimarika. Kwa wakati huu, kila kitu ni kigumu zaidi. Kwa klabu kama Manchester United kupoteza 3-0 nyumbani, ni ngumu sana kwa kila mtu. Na bila shaka mashabiki wamekata tamaa."

„Lazima tuboreshe aina ya uchezaji wetu.

„Tunafanyia kazi hilo na tutaboresha hilo pia, lakini hatukupoteza kwa sababu ya kucheza vibaya.

"Tunapoteza kwa sababu tunatengeneza nafasi nyingi na hatukufunga. Kisha, wakati huu ambapo kila kitu kiko kinyume, wenzetu wanafunguka na kufunga."

Baada ya kichapo kutoka kwa Spurs, Amorim alikosoa usimamizi wa mchezo wa wachezaji wake baada ya kuruhusu mabao mawili ndani ya dakika nane mwanzoni mwa kipindi cha pili.

Kichapo hicho kimewafanya United kuwa nusu ya mwisho ya msimamo wa Ligi Kuu kuelekea sikukuu ya Krismasi kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1989.

# Ange: Sitawajibu wanahabari

**LONDON, England**

ANGE Postecoglou amesema anaweza kuacha kujibu maswali kuhusu mbinu yake ya ushambuliaji na akasisitiza nia yake ya kuendelea na mtindo wake wa uchezaji licha ya kufungwa mabao 6-3 nyumbani na vinara wa Ligi Kuu England, Liverpool.

Matokeo hayo yanawafanya Spurs kushika nafasi ya 11 kwenye msimamo wakiwa wameruhusu mabao 15 katika mechi sita zilizopita kwenye michuano yote.

Na Postecoglou aliulizwa kama kuna sababu nyingine katika kukosa kupoteza mechi ukiacha majeraha ya wachezaji muhimu kama mlinda mlango Guglielmo Vicario, mabeki Micky van de Ven, Cristian Romero, Ben Davies na Destiny Udogie.

"Unajua nini? Nitaacha kujibu maswali haya," alisema bosi huyo wa



Spurs akiiambia BBC Sport.

"Kama watu hawawezi kuona dhahiri, sitaelezea. Angalia, fanya kile unachotaka, ndio tunaruhusu mabao.

"Sijui niseme nini tena. Nadhani watu hufanya maamuzi kwa njia yao wenyewe. Wanafikiri ninachofanya ni kizuri au hawaoni na ni sawa."

"Nadhani nimekuwa mvumilivu sana kwa muda wa miezi 18 iliyopita kuketi hapa nikijibu maswali yale yale.

"Kama watu wanataka nibadilishe mtazamo wangu, hautabadilika, tunafanya kwa sababu fulani, tunafanya kwa sababu tunadhani itatusaidia kupata mafanikio.

„Ikiwa watu hawaelewi hali tuliyo nayo kwa sasa, basi sitaji tena maswali yetu."

# BACCA KINARA WAPACHIKA MABAO MABEKI LIGI BARA

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya kupachika mabao mawili katika mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Prisons uliochezwa kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam juzi, Ibrahim Hamad ‚Bacca', anaongoza kwa kufunga mabao mengi kwa upande wa mabeki wa ligi hiyo.

Bacca ambaye ni beki wa kati ya Yanga, alipachika mabao dakika ya 42 na 83 na kuongoza Yanga kuiadhibu Prisons, kwa ushindi wa mabao 4-0, sasa amefikisha magoli manne kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, akiwa anaowaongoza wenzake wanaocheza nafasi ya ulinzi kwa kufunga mabao mengi.

Mabao mengine mawili alifunga dhidi ya KenGold, mechi iliyochezwa kwenye Uwanja wa Sokoine jijini Mbeya Septemba 25, mwaka huu na mabingwa hao watetezi wakishinda bao 1-0.

Oktoba 3, mwaka huu ndani ya Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam, akichangia ushindi wa mabao 4-0 dhidi ya Pamba Jiji alifunga bao lingine.

Mabeki wanaofuatia ambao wamefunga mabao mawili mawili kila mmoja ni pamoja na Shomari Kapombe na Fondoh Che Malone wa Simba, Anthony Trabita (Singida Black Stars), Erasto Nyoni (Namungo) na Nicolaus Gyan wa Fountain Gate.

Jumamosi iliyopita kwenye Uwanja wa Kaitaba, Bukoba, Kapombe, beki wa kulia, alifunga bao timu yake ikapata ushindi wa mabao 5-2 dhidi ya wenyeji Kagera Sugar, kabla ya hapo alipachika bao lake kwa kwanza Oktoba 25, mwaka huu, kwenye Uwanja wa KMC Complex, Simba ikicheza dhidi ya Namungo na kushinda magoli 3-0.

Che Malone ni beki wa kati, raia wa Cameroon, alifunga bao la kwanza alilifunga Agosti 17, mwaka huu kwenye Uwanja wa KMC Complex wakati Simba ikiizamisha Tabora United mabao 3-0 huku lingine akipachika Oktoba 22, kwenye Uwanja wa Sokoine na Mnyama kuondoka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Prisons.



Kiungo wa Geita Gold FC, Ada (kushoto), akiwania mpira dhidi ya mchezaji wa Mbeya City katika mechi ya Ligi ya Championship iliyochezwa kwenye Uwanja wa CCM Sokoine jijini Mbeya juzi. Mbeya City ilipata ushindi wa bao 1-0. **PICHA: MTANDAO**

# Serengeti Boys vitani CECAFA

**Na Somoe Ng'itu**

TIMU ya Soka ya Taifa ya vijana wa umri chini ya miaka 17 (Serengeti Boys), inakutana na Sudan Kusini katika mechi ya kusaka hatua ya nusu fainali ya mashindano ya Afrika Mashariki na Kati (CECAFA U-17), itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Nakivubo jijini Kampala, Uganda.

Mashindano hayo ni maalumu kwa kupata wawakilishi wa CECAFA katika Fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON U-17), zitakazofanyika Machi, mwakani nchini Morocco.

Serengeti Boys ilimaliza hatua ya makundi ikiwa ya pili wakati Sudan Kusini iliongoza katika Kundi B.

Kocha Mkuu wa Serengeti Boys, Aggrey Morris, aliliambia gazeti hili wachezaji wake wako tayari kwa mchezo huo na wanaamini watafikia malengo.

Beki huyo wa zamani wa Taifa Stars na Azam FC, alisema wamejipanga kukutana na ushindani kwa sababu timu zote zilizoingia hatua ya nusu fainali zina wachezaji wenye viwango vizuri.

Mechi nyingine ya hatua ya nusu fainali ya mashindano hayo itawakutanisha wenyeji Uganda dhidi ya Somalia.

Fainali ya mashindano hayo yanayosimamiwa na CECAFA itafanyika Jumamosi.

## Ramovic: Wachezaji Yanga wananielewa

INATOKA UK. 24

ukiangalia ni kama wachezaji wangu waliingia wakiwa na presha, ni hali ya kutojiamini, tukawa tunapoteza pasi zisizokuwa na sababu, ukikutana na timu yenye wachezaji makini, wenye uwezo ni lazima wakuadhibu.

Kipindi cha pili baada ya maelezo kwenye vyumba vya kuvalia, hali ilibadilika ikawa nzuri, lakini tukaruhusu tena bao moja kwa makosa binafsi ya mchezaji likawa la nne," alisema.

Ligi Kuu Bara inatarajia kuendelea tena leo kwa Simba kuwakaribisha JKT Tanzania huku Singida Black Stars ikiwaalika KenGold kutoka Mbeya.

Mabingwa watetezi, Yanga wao watashuka dimbani kesho kucheza dhidi ya Dodoma Jiji kwenye Uwanja na Jamhuri wakati keshokutwa Prisons itawaalika Pamba.

## Simba, JKT Tanzania kazini Ligi Kuu Bara

INATOKA UK. 24

Akizungumzia juu ya siku za karibuni timu yao kuruhusu mabao mepesi, alisema wamekaa na wachezaji pamoja na kulifanyia kazi suala hilo mazoezini na hawafikirii kuona litajitokeza tena.

„Ni kweli, tumekuwa tunapata matokeo mazuri, lakini tumekuwa tukiruhusu mabao, sisi kama benchi la ufundi hatufurahishwi mwenendo huo, tumekuwa tukilifanyia kazi, naamini kwenye mchezo huu halitojitokeza tena," aliongeza Matola.

Naye Kocha Mkuu wa JKT Tanzania, Ahmad Ally, alisema wamejiandaa vyema kuwakabili Simba, huku akiisifia timu hiyo na mwalimu wao, Fadlu Davids, wameifanya kuwa tishio katika ligi kwa sasa.

„Tumpe pongezi Kocha Fadlu kwa kuitengeneza timu nzuri, ina vijana wengi ambao ndiyo kwanza msimu huu wameingia katika kikosi, iko vizuri kwenye kila kitu, ikiwa na mpira, ikiwa haina, inakabia juu muda mwingi, mawinga hao ni balaa, kwenye kona, faulo pia ni hatari kwa hiyo tunajua tunakwenda kukabiliana na hali hiyo.

Lakini ili uwe bora ni lazima ukutane na timu bora pia, hata mwalimu mzuri lazima ukutane na yule aliye zaidi yako, tulichojiandaa nacho sana ni vipi tucheze wakati tuna mpira na jinsi ya kucheza wakati hatuna mpira, tunajua tunakwenda kucheza na timu bora, unaona wanaweza kupata matokeo popote pale, wakicheza nyumbani hata ugenini, hivyo katika mchezo huu tunataka kuwa wa kwanza katika kila tukio ili tuwe na mchezo mzuri," kocha huyo alisema.

JKT Tanzania haijapata ushindi wala kufunga bao katika michezo mitatu mfululizo iliyocheza ya ligi hiyo.

Michezo
Jumanne Desemba 24, 2024
Nipashe

Mbappe: Nitafanya mazuri zaidi Madrid UKURASA 21





Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Dk. Hussein Mwinyi (kulia), akizindua jiwe la msingi kwenye ujenzi wa viwanja vipya vya michezo vya Maisara (Maisara Sports Complex), vilivyopo katika eneo la Wilaya ya Mjini, Mkoa wa Mjini Magharibi visiwani humo juzi. Huo ni mwendelezo wa shamrashamra za miaka 61 ya Mapinduzi ya Zanzibar. **PICHA: IKULU ZANZIBAR**

# RAMOVIC: WACHEZAJI YANGA WANANIELEWA

## Kocha huyo atamba ndio siri ya kutoa dozi kwa wapinzani...

**Na Adam Fungamwango**

BAADA ya timu yake kupata ushindi mnono, Kocha Mkuu wa Yanga, Sead Ramovic, amesema tayari wachezaji wake wameanza kumwelewa nini anataka na kuongeza pia wako vyema katika utimamu wa mwili unaowafanya watekeleze kwa usahihi kile anachowaagiza.

Yanga ilipata ushindi wa mabao 4-0 katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Prisons na kufikisha pointi 33 na kuifanya ipande hadi nafasi ya pili kwenye msimamo, nyuma ya Simba yenye pointi 34 kibindoni.

Akizungumza baada ya kumalizika kwa mechi hiyo ya juzi, Ramovic, alisema ana furaha sana kwa sababu wachezaji wake wameanza kuelewa mfumo ambao amekuwa akiuingiza katika kikosi chake.

Ramovic alisema timu hiyo itaendelea kuimarika kwa sababu amefanikiwa kubadilisha mfumo wa timu na sasa mashabiki na wanachama wa timu hiyo watarajie furaha.

„Nadhani wachezaji wangu sasa wameanza kunielewa nini nataka, nina furaha sana kwa sababu namna ambavyo tunafanya mazoezi ndivyo wanavyocheza uwanjani, kilichobaki nahitaji kuona ni mchezaji gani katika kikosi changu anajituma zaidi uwanjani,“ alisema Ramovic ambaye ameiongoza Yanga kushinda mchezo wa tatu wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Aliongeza anafurahi kuona afya za nyota wake zimerejea vyema na wako tayari kucheza soka la ushindani.

„Wachezaji wangu pia wameanza kuwa na utimamu wa mwili, ukiwa fiti unakuwa na uwezo wa kutekeleza kile ambacho umeagizwa kukifanya uwanjani, kama huna hali inakuwa tofauti,“ Ramovic alisema.

Pia aliwapongeza wapinzani kwa kuonyesha mchezo mzuri, huku akisema bado ana kazi ya kufanya ili kuendelea kukiboresha kikosi chake.

Naye Kocha Msaidizi wa Prisons, Shaaban Mtupa, amesema idadi kubwa ya wachezaji ambao ni majeruhi katika kikosi chake inawavuruga na kusisitiza ni lazima waingie sokoni kwenye kipindi cha dirisha hili dogo la usajili.

„Changamoto kubwa kwetu tumekuwa na lundo la wachezaji majeruhi, kama kina Samson Mbangula, Jeremiah Juma, Jumanne El Fadhili, Salum Kimenya, Mussa Haji, Aboubakar Ngaliema, sasa tumeanza kuingiza vijana wengine bado si wazoefu inachukua muda, nafikiri inabidi turudi sokoni kutafuta wachezaji, dirisha dogo limefunguliwa inabidi tutafute wachezaji wa kuisaidia timu hii iende mbele. Tuna shida kwenye ulinzi, ushambuliaji na hata upande wa straika,“ alisema.

Kuhusu kichapo hicho, Mtupa alisema hawakutegemea kupata matokeo hayo, huku akiongeza mabao mengi waliyoruhusu ni makosa ya wachezaji binafsi na si kitimu.

„Hatukutegemea matokeo haya,

INAENDELEA UK. 23

## Simba, JKT Tanzania kazini Ligi Kuu Bara

**Na Faustine Feliciane**

KAZI moja ya kuvuna pointi tatu muhimu ndio kitu pekee ambacho Wekundu wa Msimbazi wanakihitaji kuelekea mechi ya Ligi Kuu Bara dhidi ya ‚Maafande‘ wa JKT Tanzania itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa KMC Complex, Dar es Salaam.

Mechi hiyo ni ya kiporo kufuatia kikosi cha JKT Tanzania kupata ajali walipokuwa wanarejea nyumbani Dar es Salaam wakitokea Dodoma.

Akizungumza jijini jana, Kocha Msaidizi wa Simba, Selemani Matola, alisema wataingia uwanjani wakiwa na malengo ya kuendeleza kasi ya ushindi ili kujiimarisha katika msimamo wa ligi hiyo inayoelekea mwisho wa mzunguko wa kwanza.

Matola alisema wanawaonya wapinzani wao JKT Tanzania kutoingia dimbani kwa kuwadharau kwa sababu wao wameimarika na hawako tayari kuona wanapoteza pointi katika mechi hiyo itakayochezwa kuanzia saa 10:00 jioni.

Kiungo huyo wa zamani wa Simba ameweka wazi kikosi chao kitakuwa kinabadilika kiuchezaji kutokana na namna mpinzani wao atakavyocheza, hivyo kamwe JKT Tanzania wasiingie kwa kukariri mfumo wao.

Kocha huyo alisema lengo na mpango mkakati wa kubadilisha mfumo ni kutaka kuwavuruga wapinzani ili wasifahamu walichoelezwa na makocha wao.

„Tutaingia uwanjani tukiwa na lengo moja tu la kusaka ushindi, tutaingia na mpango mkakati wetu, lakini tutakuwa tunabadilika kadri wao watakavyokuwa wanabadilika na hii itawachanganya kwa sababu kile ambacho walikifanyia mazoezi jinsi ya kutuzuia, watakutaka na kitu tofauti,“ alisema Matola.

Hata hivyo alikiri kuwa mchezo utakuwa mgumu kutokana na aina ya mpinzani ambaye wanakwenda kukutana naye.

„Haitakuwa mechi rahisi, JKT Tanzania ni moja kati ya timu bora sana kwenye ligi hii, pamoja na walikuwa hawana matokeo mazuri lakini wamekuwa na kiwango kizuri uwanjani, wana wachezaji ambao wanaifahamu vizuri ligi yetu hapa,“ alisema nyota huyo wa zamani wa Super Sport ya Afrika Kusini.

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >